# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report Of

# DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, COAST PROVINCE - GARSEN AT GARSEN METHODIST CHURCH

ON

15TH OCTOBER, 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, GARSEN CONSTITUENCY, HELD AT GARSEN METHODIST CHURCH ON 15TH OCTOBER, 2002**

**Present:**

Com. Prof. I.A. Salim
Asst. P.O. William Opili

**Secretariat Staff in Attendance:**

Gladys Osimbo – Verbatim Recorder
Leonard Loya – District Coordinator

**Committee Members:**

Sera Wande
Mrs. Eunice Mungatara
Mrs. Hadja Giyo
Muhamel Gowle
Said Rhova
Erastus Buko
Danson Buya Mungatana - Delegate

The meeting started at 10.45 am with a Muslim prayer led by Sheikh Musabals. The District Coordinator, Bernard Goya, introduced committee members.

**District Coordinator:** Wananchi wa Garsen Constituency, nafikiri sasa tutaanza rotiba yetu ya leo, ilikuwa tuanze saa nne sasa ni saa tano. Tumechelewa tuko nyuma saa nzima kwa hivyo hatutangojea zaidi, na tutaanza kwanza na maombi, tukimaliza tutamwalika Chief maanake Bwana DO hayuko, tutamwalika Chief kwa sababu huyu ni mtu wake atusalimie halafu tutaendelea. Kwa hivyo tupate Sheikh atuanzie mkutano kwa maombi.

**Prayer:** In Arabic. *(inaudible)*

**District Coodinator:** Haya sasa naona tuko tayari kuanza. Nitaanza na kujijulisha, kuwajulisha wale ambao wako hapa mbele kidogo. Kwanza nitaanza na kamati yangu. Tafadhalini wale wanakamati simameni. Hebu nataka wewe mwenyewe uzungumze, uje hapa useme jina lako useme wewe ni mwanakamati wa wapi.

**Hadija:** Hamjambo wananchi na jamii? Mimi ni wa Garsen Constituency akina mama wa upangaji wa Katiba. Hadija Mariam Kandie.

**Erasto Mbuko:** Mabibi na mabwana, hamjambo? Ma-commissioner, waheshimiwa na wananchi watukufu, leo tunakuja hapa kwa sababu ya mambo yenu. Mimi ni Chairman wa Katiba katika Division hii. Wenzangu kwa sababu ya shuguri ya mvua hawaja aja sasa niko na huyu mama na Sera Wande lakini natumaini kwamba wengine watakuja. Kwa hivyo mimi naitwa Erasto Mbuko, Councillor wa Salama Location.

**District Coordinator:** Asante sana, tuko wengine hawajafika, lakini kuna huyu mama hapa na huyu mzee ambaye pia ni Councillor, kuna yule mama Sera Wande ambaye ametoka ataingia, mama wa Maendeleo. Kuna wengine ambao hatukuwapata na hapa pia tunao wageni wengine wamekuja tu, tumewaalika kuangalia mambo ya public service yetu. Lakini mgeni ambaye niko naye hapa nashugulika naye sana katika mipango hii ya kuwaita wananchi ni Chief. Sasa nafikiri yeye nitamwalika aseme neno kwa ufupi tu kwa maana tumechelewa, kwa hivyo akisimama mwenyewe atasema jina lake na atatwambia machache. Na kwa hivyo sasa kabla sijaendelea nitampa nafasi Chief, azungumze kidogo, kisha awaalike wageni na watajijulisha wenyewe. Karibu.

**Chief Abdalla:** Commissioner, Bw. Mungatana, wazee wote waliokuja, hamjambo tena? Mimi nasimama hapa kwa niaba ya DO wetu wa Garsen, alikuwa na safari na hata leo asubuhi alipiga simu, aliomba ladhi Bw. Commissioner kwa kutokuwa hapa. Kwa hivyo kuja kwenu tulitalajia leo mtafika, na naona saa hii watu hawajafika kwa wingi lakini saa hii tumepita hapa mjini na tunawajulisha kwamba mmeshafika lakini tatiso kidogo ilikuwa hii mawingu na wenyeji wa hapa wengi ni watu wanokaa kando kando ya hapa mji wa Garsen. Kwa hivyo tunaomba ladhi kwa kuchelewa kufika hapa watu wengine watakuja saa hii. Kwa hivyo tunawakaribisha hapa kwetu Garsen ili muweze kuendelea na ile shuguri. Asanteni sana. Jina langu naitwa Abdalla Bakaro, Chief wa Bilisa Location.

**Com. Salim:** Asante sana Bw. Chief kwa kutukaribisha, tumefurahi kuja hapa kwa kazi hii mhimu sana ya kuwaeleza yaliyomo katika mzwada wa katiba mpya ambayo Tume yetu ilitayarisha. Mimi jina langu ni Ahmed Idha Salim, mimi ni mwanatume na pia ndie makamu wa mwenyekiti wa Tume. Kutoka Nairobi nimekuja na wenzangu wawili na wako pale wako na shuguri ya kuandika moja wao ni Gladys na mwenzake William. Hao wako na kazi muhimu sana. Kazi yao ni kuandika yote ambayo yatasemwa leo, na pia kunasa kwenye tape maneno yatakayosemwa. Na hii ni muhimu sana ili tukirudi Nairobi tuweze kukumbuka na kujua ni ipi ambayo yamezungumzwa hapa Garsen. Si sisitu tutaosoma ama kujua iliyofanywa hapa hivi leo lakini pia visazi vijavyo. Wanarecodi tume recodi zote zake zitakuweko na zitawekwa, zitahifadhiwa ili kwamba baada ya

miaka ishirini, thelathini, hamsini na mia moja; yeyote ambaye ana interest ya kujua au anahamu ya kujua kulitokea nini kati ya Kenya kati ya mwaka fulani na fulani ataweza kwenda akasoma na pia kusikiza tape akitaka. Kwa hivyo watoto wenu na watoto wa watoto wenu huenda siku moja wakafanywa uchunguzi katika jambo hili kubwa ya kihistoria ilitokea hapo Kenya ya kujaribu kurekebisha katiba yetu.

Sina haja ya kurudi nyuma sana kama mlivyo elezwa tumepoteza saa nzima, ilikuwa tuanze saa nne, sasa tunaanza saa tano na kitu. Lakini kwa ufupi mnajua kazi yetu hii ya tume yetu ni kurekebisha katiba kuitengeneza iwe bora zaidi. Kwa nini iwe bora zaidi? Ili kuinua na kushtawisha hali ya kila Mkenya, apate hali ya kijamii, hali ya kiuchumi hali ya kisiasa pia iliyo bora zaidi, na pia apate uhuru mkubwa zaidi. Na kama nitavyoeleza katika yalimo hapa katika mzwada wa katiba mtaona kwamba mabadiriko tuliyo sisi pendekeza ni makubwa sana katika maeneo fulani.

Na kabla ya kuiandika hii katiba mnakubuka tulizunguka nchi nzima ama tume nzima au vikundi vya watu watatu au wanatume watatu au wanne, tukitembelea kila constituency, tukakusanya maoni yenu. Na madhumuni ya kukusanya maoni yenu juu ya kurekebisha katiba, ili tuhakikishe kwamba tukishaa irekebisha au kazi hiyo ya kuirekebisha inategemea maoni ya wananchi. Na kwa hivyo mimi naweza kusema kwa yakini kabisa bila kusitasita, hii katiba imerekebishwa kufuatia maoni ya wananchi, wala haikurekebishwa sisi wenyewe katika akili zetu ya wanatume tukaka tukaandika tu bila kuzingatia maoni ya wananchi. Hiyo ndiyo background ama kinyume cha kazi yetu hii tunayofanya.

Katiba hii ilitolewa kabla ya siku chache tu, kabla ya hapo tulitoa pia taarifa au repoti ya kazi yetu jinsi ambavyo kazi hii ilifanywa. Sijui Bw. District Coordinator ulipokea nakara ya hiyo ripoti? Ulipokea pia nakara ya mswaada wa Constitution? Wapi? Sasa ziko wapi? Maana sioni mmoja yeyote alikuja nayo leo ili kuirudia ndiyo kujua saa ile nazungumza, nazungumzia jambo gani?

**District Coordinator:** Haziwezi kutosha hizi lakini zilikuwa chache na zile zingine sitakuja.

**Com. Salim:** Na zile za magazeti?

**District Coordinator:** Zile za magazette ndizo nimewapatia tu saa hizi.

**Com. Salim:** Nani hajapata nakara iliyomo kwenye magazettee? Mnazo? Lakini sizioni maana tutazungumzia mengi lakini mkiwa nazo mtakuwa mkirudia mkajua mengi, so and so, kulasa so and so, mimi nazungumzia kurasa huu hebu tazameni mtaona hivi na yale. Hata hivyo hebu niendelee kuhakisha kwamba tunataja mambo yaliomuhimu. Kwa hivyo kuna mambo nne iliyorekebishwa.

Kwanza kuna report ya kazi yetu jinsi tulivyofanya tukasikiza maoni ya wananchi, mwananchi akatwambia kitu gani na jambo

hili ama lile au swala hili au swala lile kisha tukaandika huu mswaada wa Constitution. Mswaada huu wa Constitution kwanza maana yake ni draft, jambo ambalo limeandikwa hapa kama pendekezo ili baadaye lipitie kwa njia ya kisheria linageuzwa kuwa kanuni. Kwa hivyo hapa tuna mswaada wa kanuni mpya au mswaza wa katiba mpya. Hapa kuna mapendekezo, tunasema ifanye hivi ifanywe hivi ifanywe vile, lakini si maanake kwamba mwishowe tutapata katiba hii, kama ilivyo hapa. Maana baada ya sisi kuwaeleza kuwakuwa mwezi huu utakaraji kuwakuweko mkutano mkubwa sasa, mgogomano wa watu zaidi wa mia sita- kati mia sita na mia saba. Watu hawa watakuwa ni wakilishi wa wananchi. Kati yao watakuwemo wabunge wote zaidi ya mia mbili vile mjuavyo. Kisha kutakuweko waakilishi watatu, kutoka kila district au wilaya. Kila wilaya itapeleka wajumbe watatu ambao wamekwisha chaguliwa. Kisha kutakuwa na viongozi wa kidini. Kila ndini itapeleka viongozi kwenda kusikiliza na kushiliki katika kujadiliana juu ya hii katiba mpya tulioandika. Pia kutakuweko wajumbe wa akina mama, wajumbe wa walemavu, wajumbe wa vijana n.k. Ili kwamba katika mkutano huu kila section ya wananchi wa Kenya na wajumbe kujadili juu ya hii katiba. Watajadiliana na tuombe kwamba mwishowe itapatia kama ilivyo bali na mabadiriko machache hapa na pale. Lakini ata hivyo mabadiriko yale itatokea kutokana na majadiliano ya huo mkutano mkubwa yatatiwa katika hii katiba. Itaandikwa vingine kufuatana na mapendekezo ya mkutano huu mkubwa kule Nairobi – Bomas of Kenya. Sawa? Tutaandika vingine kisha ndiyo itapelekwa bunge na bunge itaipitisha iwe ni katiba yetu mpya. Kwa hivyo hatujamalizana nayo.

Tumeandika mswaada, draft lakini huenda hii draft ikabadilishwa hapa na pale kufuatana na hawa wajumbe wetu wa mia sita na kitu ambao wataizungumzia na kujadiliana juu yake. Sasa huu mswaada kama mambo yalivyo hapa, mapendekezo yaliyomo hapa, tungependa kuwaeleza yale ambaye ni mhimu. Sina wakati wa kuwaeleza kila jambo lililoko hapa. Itakuwa ni waajibu wa kila mtu ambaye ana hamu ya kujua kuenda kuchukua mswaada huu akaisoma yeye mwenyewe, kuifahamu zaidi. Kuna ya Kiingereza, na pia ilitolewa hivi karibuni katika gazete la taifa, tafsiri ya mswaada huu kwa lugha ya Kiswahili pia. Kwa hivyo mnaweza kuulizana na mwenye ako nayo yule ambaye anahamu ya kutaka kujua yaliyomo anaweza akajipatia akasoma yeye mwenyewe.

Mswaada huu una sura ishirini, chapters ishirini. Kwa hivyo njia ambayo nitaifuata mimi ni kueleza yale yaliyo mhimu kabisa katika huu mswaada ya kupatia sura baada ya sura. Sina wakati wakumaliza kila sura. Nitaacha mengine nitashikiria yale ambayo ni mhimu kabisa lakini hayo ni mengi zaidi kwa hivyo majority ya sura nitayapitia sasa na nyinyi mnisikize uzuri kisha ikiwepo kuna jambo ambalo nitaeleza kiwazi wazi mtaniuliza baada ya mimi tu kwisha kueleza. Nitaendelea kwa muda labda muda wa saa mbili, maelezo hayo yatakuwa marefu, ili kuhakikisha kwamba kila moja wenu anapata haki yake, ya kujua tumeaandika kitu gani katika huu mswaada, ili tusije tukalaumiana baadaye kwamba mimi sikusikia jambo lolote juu ya hili au lile. Na tafadhalini nitaachia thaluthi ya wakaaji nyinyi wenyewe mtaniuliza au kutoa maoni yenu wale ambao wamepata nafasi ya kuipitia. Sawa hivyo? Tuendelee. Bisimilahi.

Kama nilivyosema kuna sura ishirini hapa na tunaanza na Kitangulizi, Preamble inaitwa kwa Kiingereza. Kitangulizi ni kitu mhimu katika kila kitabu, katika kila kitu ambayo inaandikwa maana ile kitangulizi mtu akisoma akiaanza anajua tunaanzia

jambo gani katika kile kitabu hiki kinaitwa constitution. Constitution ama katiba tulionayo sasa haina kitangulizi inaenda moja kwa moja katika sura ya kwanza. Lakini sisi tumeona na tulipendekezewa na wananchi tuwe na kitangulizi kwenye hii katiba mpya. Hata wananchi wengine walisema tieni vitu hivi, wakatusomea aina vitu bali bali vya vitangulizi ambao ninapendekeza viwemo hapa. Sisi mwishowe tukaanza kuzingatia mapendekezo ya wananchi na tukaandika hii iliyoko sasa. Sijui nisome Kiingereza ama Kiswahili? Tafsiri yake? Iko kwa Kiingereza lakini hebu niwatafusirie, sina ile copy ya ule mswaada ya Kiswahili lakini kwa ufupi kitanguli inasema hivi:

Sisi raia wa Kenya, niseme ni mhimu sana maana hii katiba ni ya wananchi wananchi ndiyo walitoa mapendekezo hayo na kutaka kusema aina ya serikali tutakayo, aina ya uchumi tutakayo. Hii inaitwa "people driven Constitution" ilipelekwa mbele kama gari na wananchi mpaka ikafika hapa. Kwa hivyo tunaanza na hii statement ambayo utaona kwamba katiba ya nchi nyingi sana inaanza hivyo. We the people of Kenya, maana watu wa Kenya, raia wa Kenya ndiyo mabwana wa nchi ya Kenya; raia ndiyo mabwana wa nchi hii. Kwa hivyo inasema sisi wananchi wa Kenya, tukiwa tunamiliki tofauti zetu za kikabira, kiutamaduni, na za kindini, na tukiwa na nia ya kuishi pamoja kwa amani na umoja kama taifa moja isiyo gawanyika. Tukiwa na heshima kubwa ya kustawisha na kurinda hali nzuri ya kila moja wetu, kila familia yetu na kila jamii yetu. Pia tukitambua matakwa ya akina mama, wanaume, na kupata serikali ambayo msingi wake ni maadhiri ya kidharura ya uhuru, democrasia, uadhirifu ya kijamii na utawala wa kisheria. Haya ni maadiri, (values). Pia tukitumia haki yetu sisi wananchi ya Kenya ama raia wa Kenya tukitumia haki yetu ya ufalme wetu, our sovereignty na haki yetu isiyoweze kuchukuliwa na yeyote kuchagua aina ya serikali tunayopendelea nchi yetu kuwa nayo. Na kwa kuwa tumeshiriki katika kazi ya kurekebisha hii katiba sisi wananchi wa Kenya au raia wa Kenya, tumekata shauri kuipokea kuifanya ni sheria yetu na kuipa nafsi zetu katiba hii sisi wenyewe. Na pia kuipa katiba hii vizazi vyetu vijavyo. Mungu aibariki Kenya. Hiki ni kitangulizi, nafikiri mmeifahamu hapo, tumeandika hivyo. Umhimu ya raia, umhimu wa raia kusema ni aina gani ya serikali wanataka, na kusema hii ni katiba yao na kwamba wao wanajiipa hiyo katiba na pia kuipa vizazi vijavyo.

Baada ya kitangulizi tunaingia sura ya kwanza. Sura ya kwanza ya katiba hii inaitwa Sovereignty of the people and supremacy of the Constitution. Sovereignty of the people maana yake ni neno muhimu kujua haki, lakini sovereignity of the people ni watu ni kuwa au raia kuwa ni kama ufalme. Ufalme wa watu. Sovereignty of the people. And supremacy of the Constitution maanake ni Katiba kuwa juu ya kila kitu, supreme. Na kama mjuavyo Katiba kwa hakika ni sheria kubwa kabisa katika nchi yeyote. Sheria zote nyingine na mwanasheria yuko hapa, sheria yeyote ingine lazima iwe inalingana na katiba. Ikiwa kuna sheria yeyote ambayo inatengana na yalimo katika katiba basi sheria hiyo sio ya halali. Na ikiwa jambo lolote litafunjwa katika hii katiba pia mtu anaenda kortini akaenda akachukua mwana sheria kumtetea. Haki yangu ambayo iko katika katiba hii yetu imevunjwa na kanuni nyingine ambayo imetoka kwingine. Kwa hivyo utaona kwamba baada ya hii katiba kuandikwa na kukubaliwa kutakuwa na sheria nyingi zingine ambazo zitabadirishwa, sheria nyingi zitabadirishwa kulingana na katiba. Hiyo ndiyo ikaitwa supremacy of the Constitution. Sawa? Mtasoma wenyewe haswa tunasema nini habari ya supremacy ya hii Constitution.

Tukiendelea mbele ukurasa wa sura ya pili inaitwa the Republic, Jamhuri. Tunaelezwa sisi Kenya ni Jamhuri, tunazungumza juu ya jamhuri ya Kenya. Katiba tulieyenaye sasa inasema kwamba Kenya itakuwa Jamhuri. Lakini tunafahamu maana ya kuwa jamhuri. Nini maana ya kuwa jamhuri? Kwa hivyo hapa tunaeleza. Jamhuri ya Kenya au Kenya itakuwa Jamhuri na itaendeshwa itaotawaliwa kufuatia maadiri ya Jamhuri au maadiri ya Kijamhuri. Maadiri hiyo ni nini? Values hizo ni nini? Values hizi ni utawala mzuri kufuatia siasa ya viama vingi, multi-party democracy, maadiri moja hayo. Yaani maadiri yetu itapelekwa kufuatia kuweko vyama vingi vya kisiasa, si chama kimoja kinachotawala na ambacho kinazuia kuweko na vyama vingine vya kisiasa.

Pia maadiri mengine ni utawala ambao unashilikisha wananchi katika utawala huo, participatory governance. Utawala wa kushiliki wananchi. Maana jamhuri, neno hili jamhuri kwa hakika ni neno la Kiarabu, Jamhuri, watu, raia, taifa, raia wote wa Kenya hao ni Jamhuri, the masses. Na aina hii ya Serikali iko tangu zamani tangu siku za Ungiriki, Wangiriki walikuwa wakitawala na walikuwa na republicans form of government. Kwa hivyo utawala unaoshirikisha wananchi ni maadiri ya pili ambayo ningependa ku… Pia itakuwa ni Serikali ambayo ni wazi, transparent. Lazima iwe serikali yake ni transparent unaweza kuona jinsi ambavyo serikali hii inafanya kazi yake. Hakuna mambo ya kufichwa ya kufanywa kisiri siri. Na pia accountability, maadiri ya accountability, maadiri ya mtu kufanyiwa hesabu, mtumishi wa Serikali mkubwa mdogo anafanyiwa hesabu na wananchi. Wale ambao wanadini ya Kikristo na Kiislamu wanajua kwamba Mwenyezi Mungu atakufanyia hesabu siku ya kiama unafanyiwa hesabu na Mwenyezi Mungu wewe ulifanya hivi na hivi bona hukufanya hivyo. Wewe uliatakikana ufanye hivi ulifanya hivyo au hukufanya? Kwa hivyo Serikali yetu itakuwa Serikali ambayo ni accountable to the people kwa rais atafanyia hesabu Serikali hiyo. Kwa hivyo maadiri ya accountability ni muhimu katika Serikali ya jamhuri yeyote.

Pia Serikali ambayo itaheshimu haki za kibinadamu, uhuru wa kimsingi wa kila raia, na utawala wa kufuata sheria. Unaweza kufuata utawala ambao haufuati sheria, kunatawaliwa tu kama serikali ya kikoloni. Ilifuata sheria? Haikufuata sheria. Kwa hivyo sisi tunasema jamhuri yetu pia iwe inaheshimu haki za kibinadamu za kila mmoja wetu. Nitaeleza baadaye haki hizo ni zipi na pia itafuata sheria. Itatuhukumu kwa njia ya sheria. Sheria ambayo tunaijua pia ambayo tutaisoma na kujisomesha na pia kwa ufupi ndiyo chapter 2 au sura ya pili ndiyo tumezungumzia kwa hayo. Na tunaeleza kwa sura hivyo kwamba mipaka ya Kenya itakuwa ni ipi, mtasoma hapa mipaka yetu itakuwa ni ipi kwa urefu na kwa ukamilifu. Pia mnajulizwa kwenye kulasa hii kwamba mji wetu mkubwa utakuwa ni Nairobi, kuwa kutakuwa na serikali ya Bunge, ambayo itatutengezea sheria ambayo itatufaa katika mambo tofauti tofauti. Tunasema pia katika sura hii kwa lugha yetu ya kirasmi ni mbili Kiswahili na Kiingereza. Lakini lugha halisi ya kitaifa ni Kiswahili. Sawa? Haya yote yako katika sura ya pili.

Sura ya tatu, inaitwa National Goals, Values and Principles. Sabaha za Kitaifa na maadiri ya kitaifa na mabadhi ya kitaifa. Kila nchi lazima iwe na lengo au malengo, msabaha sio mtu anaishi tu. Anamka anaendelea na kazi lazima tuwe na shabaha. Tunasafari ya kuenda tunaelekea kule na katika njia hii tunafanya hivi natufanye hivi, kisha tufanye hivi. Na katika hiyo safari yetu tutakuwa tukiongozwa na maadiri fulani muhimu. Kwa hivyo katika sura hii ya tatu, tumeeleza kikamilifu shabaha zetu na maadiri yetu. Mtasoma wenyewe sura hii. Kwa ufupi tunasema kwamba serikali itaendeshwa kwa njia iliyo wazi, na wafanyi

kazi wa serikali wawe wenye kuhesabiwa na wananchi. Pia tunasema kwamba Serikali ya jamhuri itaheshimu, italinda, na kushtawisha pia haki za kibinadamu na uhuru wa kina aina. Kuna uhuru wa aina nyingi. Nitaeleza baadaye. Kwa hivyo Serikali inajukumu ya kuheshimu, kushtawisha na kulinda haki za kibinadamu na uhuru wa kina aina ambao kila moja wetu kila raia amepewa tangu kuzaliwa. Amepewa na Mwenyezi Mungu kwa wale ambao wanaelewa. Tumezaliwa na haki hizo. Kila mmoja wetu ako na haki za kuishi. Siyo? Tumezaliwa na haki hiyo. Haki ya roho, haki ya binafsi. Kuna haki ya kuinuka ukaenda kule ukitaka au kuenda kule ukitaka, haki ya movement. Haki ya kusema. Kwa hivyo haki zote hizi tunasema katika shabaha zetu na maadiri yetu kwamba tuwe na haki hizo na Serikali ihakikishe kwamba haki hizo zinalindwa kwamba zinaheshimiwa. Pili zinarindwa kutoka hatari yoyote. Tatu, zinastawishwa. Haki ni kama binadamu, inastahishwa, unastawi unakuwa bora zaidi. Sio? Kwa hivyo haki zetu zinaweza kushtawisha pia. Kufanywa kuwa ni bora zaidi, na hii ni kazi ya Serikali, kushtawisha haki za wananchi.

Pili pia tatu tunasema Serikali, itaendelesha umoja wa taifa na kushtawisha hazimiyo la wananchi kuwa na roho ya uraia mkubwa zaidi. Ni waajibu wa serikali pia, kuendelesha umoja wa taifa tuendelee kuwa watu wamoja, one nation, taifa moja ya Kenya. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa umoja wetu unahifadhiwa pia. Na kwamba kila mmoja wetu anawekewa roho ya uraia. Partiriorism. Kupenda nchi yake mtu kushikamana na mwananchi mwenzake ili kushtawisha nchi. Hiyo pia ni kazi ama shabaha au lengo ya serikali yetu itakayoundwa kulingana na katiba hii.

Pia tunasema serikali itajilazimu kuleta udhalifu wa kijamii au itajirazimisha kuleta uadhirifu wa kijamii. Social justice. Udharifu wa kijamii maana yake ni nini? Sote ni jamii. Sote tukiwa pamoja ni jamii nzima. Kwa hivyo tunataka uadhirifu kati yetu. Ili kila member ya jamii iliyoko hapa, tuseme hii ni nchi yetu anahisi kwamba kuna uadhirifu katika kuendesha maisha yetu. Huyu hafai zaidi ya huyu. Mzee hapa hanyimwi haki ambayo mimi naipata. Haki zetu ziwe ni sawa. Huo ndiyo uadhilifu – justice or equity. Hilo pia ni lengo moja lililoko katika katiba. Pia tunasema kuwe na maendeleo na ustawi kwa kila sehemu ya nchi bila ya ubagusi. Na kutumia mali ya uma, au mali ya taifa kwa uzuri inao...

Katika kuzunguka hapa na pale tumeelezwa kwingine wananchi wanalalamika, hii district iko hapa mbele ina barabara nzuri, kilimo kinastawishwa huko na sisi hapa tunamifugo lakini hatuna soko la mifugo, barabara zetu pia ni mbaya. Hatuwezi kupeleka mifugo yetu mbele ili kuuza. Watoto wetu wanazulula hakuna skuli za kutosha. Kwa hivyo tunasema shabaha ya Serikali kufuatia maadiri haya itakuwa ni kuhakisha kwamba kila sehemu inapata ustahi sawa na sehemu nyingine ya nchi. Na kwamba mali ya umma, mali ya taifa, mali ya asili ya taifa inatumikiwa au inatumiwa kwa njia ambayo ni nzuri. Hapo tunakubaliana nafikiri. Sawa?

Pia tunasema kwamba Rais kufuatia hii Katiba, Rais, ataripoti ndani ya Bunge nakwa wananchi wote, mara moja kila mwaka juu ya hatua zilizochukuliwa katika mwaka ule, ili kushtawisha hali ya mwananchi na maendeleo yaliopatikana mwaka ule kutimisha shabaha hizi nilizozitaja. Yaani Rais atainuka kwenye Parliament mara moja, ikiwa si mara mbili tatu, lazima mara moja. Tuseme katika mwaka huu tumeweza kufanya hivi na vile. Tunampatia kila mwananchi jambo hili au lile maana hayo

ndiyo marengo na shabaha yetu na itakuwa ni waajibu wa Rais kuenda kwenye Parliament kuwambia yenye kufanyika katika mwaka ule.

Sura ya nne, inazungumzia uraia; ni nani ambaye anazingatiwa kuwa ni raia kwa Kenya. Hapa tunafanya mabadiriko fulani tofauti na yaliyomo katika katiba iliyoko. Tunasema wazi wazi kwamba, raia wa Kenya kila mmoja wao awe na haki sawa na kila mmoja wao afaidike sawa na mwenzake, asiwe raia moja anapendelewa zaidi ya raia mwingine. Pia tunasema kwamba kila raia ana wajibu wake pia, wajibu wangu ni sawa na wajibu wa mwenzangu hawa wote. Kuna haki pia kuna wajibu. Siyo? Hizo zaenda pamoja.

Pia tunasema kwamba uraia unapatikana kwa njia moja kati ya njia tatu, kwa kuzaliwa mtu. Na tunasema kwamba yeyote atakayezaliwa hapa Kenya, ikiwa mamake, au babake, ni raia wa Kenya basi huyo mtoto ni raia wa Kenya. Hana haja ya kuleta birth certificate ya nyanya ake au babu wake kabla ya kukubaliwa kuwa ni raia wa Kenya. Pia kwa registration, kuandikishwa au kushajiriwa, mtu anaweza kushajiriwa kuwa raia wa Kenya akiwa amekaa hapa Kenya kwa muda wa miaka saba, na katika muda huo anaendesha maisha yake kwa usawa na kwa njia nzuri anaweza kupeleka ombi lake na ombi lake likatazamwa na ikiwa kuna jambo lolote, pingamizi lolote ikiwa amekaa hapa Kenya miaka saba mfururizo huyo anaweza kuwa raia wa Kenya kwa kusajiriwa si kwa kuzaliwa. Na watatu atakuwa raia by naturalization, unaweza kusoma mwenyewe juu ya jambo hili. Pia tunasema kwamba, Bunge itaandikisha kanuni nyingine kufuatia kanuni hizi kushtawisha zaidi, zaidi kanuni hizi kuhusu uraia.

Kisha tunakuja kwenye sura ya tano, inaitwa the Bill of Rights. Kanuni ya haki Kama nilivyoeleza hapo awali na haki nyingi za binadamu amezaliwa na haki nyingi sana na tukasema kwamba Serikali inaweza kushindwa kurinda haki hizo. Sasa sisi hapa tumetia sura ya tano list ya haki zote raia anazo. Ni list mhimu sana. Bila urais kwa kila nchi, ni sura mhimu sana katika katiba yeyote. Maana hapa tunahaki ambazo kila mmoja wetu akinyimwa kesho atapata taabu. Na tumeisifu kidogo kusema kwamba tume yetu imeandika hizo rights, kanuni ya haki ambayo ni kubwa zaidi – too ambitious kuliko katiba za nchi nyingi hapa ulimwenguni. Tumefikiria kila aina ya haki, ya kibinadamu tumeitia hapo na mtasoma wenyewe, hii pia ni sura ndefu kwa kuwa tumetia haki nyingi sana.

Na tumesema ya kwamba Serikali itachukua hatua za kuweka sheria zinazohitajika kuwapatia wananchi haki nyingi sana. Haki moja ni haki za kimusingi. Basic Rights. Na Basic Rights au haki za kimusingi ni mhimu kwa kila mmoja wetu. Haki hizo za kimusingi ni zipi? Haki za kupata chakula, haki ya matibabu, ukiwa mgonjwa, haki ya kupata elimu ya kimsingi, ikiwa si elimu ya juu zaidi, elimu ya kimusingi kila raia wa Kenya lazima aipate. Haki ya maji masafi, maji ni maisha, au sio? Water is life. Maji ni chanzo ya maisha kwa kila mwananchi kwa hivyo tukipata maji mabaya machafu yenye madhara, yenye kuleta magonjwa tumenyimwa haki yetu. Kwa hivyo tunasema kwamba mwananchi wa Kenya lazima apate maji safi kuwa ni haki yake ya kimusingi. Haki ya makao ili kwamba kila mwananchi asilale barabarani na kado kado ya barabara au kwenye vichaka usiku. Awe na makao. Si lazima iwe ni makao mkumbwa, makao ya vyumba vitano, sita n.k. Basic need, basic

accommodation. Maskani ya kimusingi, a roof over his head asipigwe na jua, asipigwe na mvua asiliwe na wanyama n.k.

Na tunasema kwamba tunajua haki hizo za kimusingi zina gharama kubwa pia. Kwa hivyo tumesema kwingine katika hii katiba kuwa si lazima Serikali impatie mwananchi haki hizo zote za kimusingi kesho, au kesho kutwa au mwezi ujao, au mwaka ujao. Lakini Serikali ni lazima ianzishe kazi ya kumpa kila mwananchi haki hizi. Na kama nilivyosema hapo awali, kila mwaka Rais atakuwa akienda Bungeni au kwenye Radio kuwaeleza wananchi au kuripoti tumefikiria wapi kufika kumpa raia haki zake. Pia tunasema, haki nyingine ni kwamba kusiwe na ubagusi katika nchi yetu ya Kenya. Ubaguzi wa kikabira, kabira fulani, ni bora kuliko kabira fulani ubaguzi wa kijinsia, wanawake kudharauliwa, kwa hivyo haki zao wale zi lazima iwe ni sawa na mwanamume. Ubaguzi wa kiasili mimi asili yangu ni bora kuliko yako, hakuna ubaguzi wa rangi, hakuna ubaguzi ya umri, mimi ni mkubwa kwa hivyo mimi haki zangu zaidi kuliko wewe mdogo.

Ubaguzi wa uzima, mimi ni mzima wewe ni mlemavu, you are handicapped, don't expect the same rights. Usitaraji haki kama mimi mzima na ubaguzi wa ndini. Ndini yangu ni bora kuliko yako. Ndini yangu inastahili kupewa masaa mengi kuliko yako katika radio, TV kuliko ndini yako. Hakutakuwa na ubaguzi wa kindini au wa ukitamaduni wewe uko nyuma wewe uko mbele zaidi katika utamaduni au utamanduni wangu ni bora kuliko wako na au lugha. Lugha zote ni sawa. Lugha za wananchi, lugha za akina mama ni sawa katika haki hizi tuliko nazo katika hii Bill of rights.

Haki za wazee, tumezungumzia haki za wazee, tunasema kwamba wazee mara nyingi wamekuwa wakiwekwa kando, hawajaliwi na watoto saa zingine wanakimbia wazazi wao hawatunzi kwa njia inayofaa, kwa hivyo tunasema kwamba serikali iingilie. Jamii isaidie kuwatunza wazee, lakini Serikali pia isaidie kuweka wazee kwa njia ambayo ni ya heshima na njia ambayo hawatataka idhilani yeyote.

Haki za watoto, tumezungumzia kwa urefu hapa haki za watoto. Haki zao za kupata chakula za kutosha mavasi ya kutosha, kuelemishwa kutosha, kutolazimizwa kufanya kazi ikiwa hawataki. Mtoto badala ya kupelekwa shuleni anaambiwa nenda leo asubuhi ukauze mandazi, mahamri, au njugu hapa na pale azulula usiku kucha ama mchana kutwa, naye anauza badala ya kuenda shuleni. Kwa hivyo tunajua mmelezwa kwa masaa ingine ya jamii ya yule mtoto labda inadharula ya kupata mapato fulani ya kunyua maziwa na mkate kulisha jamii nzima. Kwa hivyo ule mtoto anasaidia. Lakini tunasema kwamba tukishtawisha kila kitu hali yetu ya kijamii, nchi mzima, huyo mtoto hatakuwa na haja kuenda kuzulula hapa na pale bila kusoma au kukaa barabarani na street children au watoto wa barabara na kucheza na kuingilia mambo ambayo ni mabaya kwake. Kwa hivyo tunazungumzia haki za watoto hapa kwa urefu.

Walemavu pia haki zao tumezungumza kwa urefu kwa ajili wakati sina, lakini mkiwa mnataka kuniuliza baadaye nitamueleza. Muhimu zaidi walemavu ni kwamba tuwaweke katikati ya jamii. Washiriki kwa kikamilifu. Wawe wakichaguliwa kuwa Councillors, wachaguliwe kuwa Wabunge, wachaguliwe kuwa Managers hapa na pale; muhimu ni kwamba ile kazi anaweza kufanya. Lakini umsahirishie pia ufanye kazi yake kuwa rahisi zaidi. Kwa hivi sasa utaona majengo kubwa yanayenjengewa

hapa na pale hazina lift. Mlemavu akitaka kupanda juu kumuona daktari anapanda juu kwa daraja au sio? Au kwa gazi, mshahirishie pia apande kwenye magari, utaona kuna uraya kila bus ina gazi maalum ya kumwezesha yule mulemavu kupanda ile… **end of side 1 A**…

**Side 1B**… Serikali lazima pia ichapishwe kwa ile lugha ya braille ambayo asiweza kuona kati yetu aweze kufuata mambo inayofanywa hapa nchini aweze kusoma mwenyewe bila kusomewa na mtu mwingine kwenye gazeti.

Pia tunazungumzia, haki ya kulindwa. Tunapendekeza kwamba hukumu ya kunyongwa iondolewe kwa hivyo tumesema adhabu kubwa zaidi iwe ni ya kufunga mtu kwa muda mrefu zaidi au mpaka afe. Lakini hukumu ya kuuawa au kunyongwa iondolewe lakini wananchi wengine hawapendelei jambo hili lakini ni pendekezo tu na wapi ambapo mkutano mkubwa huko Nairobi wakifika hapo huenda wakabadilisha. Kama vile watabadilisha jambo lingine lile nimelisema au nitalisema badaye.

Pia tunazungumzia haki ya ndini, haki za kidini. Kila raia ana haki ya uhuru wa kindini, fikira za kindini na maoni yake ya kindini asiingiliwe na mtu yeyote katika fikira hizo au maoni hayo. Kila raia ana haki ya kuabundu kufuatia mila au ndini atakayo au kusoma au kusomeshwa ndini hiyo. Elimu ya kindini itatolewa katika shule za Serikali na kupewa kwa njia isiyopendelea ndini yeyote. Ikiwa kuna shule za kiserikali, kuna Waiislamu, njia zitafutwe shule ya Kiislamu ishomeswe watoto Kiislamu, ile ya Kikristo isomeswe watoto wa Kikristo n.k. Kusiwe na ubaguzi wowote au mapendeleo kati ya ndini hizo. Pia raia asinyimwe haki ya kuingia shule yoyote au kutopata kazi kwa ajili ya ndini yake. Mimi ni Mkristo kwa hivyo siwezi kupata kazi hapa. Wewe ni Hindu kwa hivyo huwezi kuingia shule hii, hii ni ya Waislamu peke yao au hii ni shule ya Wakristo peke yao. Kuwe na shule za Kiserikali ambazo zitampokea mtoto yeyote bila ubaguzi wa kindini.

Kisha kuna haki ya kusema mtu maoni yake bila kuambiwa maoni hayo ni hatari ushikwe, ushtakiwe kuwa ume,… lakini kama nimesema hapo awali kila haki inawajibu wake pia, sio? Ni haki yako kusema utakayo lakini huna haki ya kusema jambo litakamuuthi mwenzako unamtukana kabira lake unatukana ndini yake, au unajaribu kusema kwa jina ambayo italeta fitina kati ya watu na watu kupigana na pia kuuwana. Kwa hivyo hapo utashtakiwa nakuathibiwa, ikiwa utatoa maneno ambayo italeta ugovi na watu kupigana au italeta chuki kati ya jamii moja au nyingine.

Haki ya kupata matibabu ni haki. Haki ya kupata elimu ni haki. Every person has a right to basic education, including pre-primary, primary, secondary education hiyo ni haki mtu anaweza kundai. Hizo haki nafikiri nimezitaja hizo basic rights elimu ya matibabu ya nyumba ya chakula na maji. Pia tumetaja haki za wateja jambo ambalo hivi sasa hatuna. Ukinunua jambo unahakika kwamba hilo jambo linastahili mali au lile bei ambalo umetoa. Sikuwa umepewa kibereti ambayo mfanyi kazi litafunjika vunjika vujika na kwenye kiti cha thelathini na viwili uanapata ni vitatu. Kwa hivyo mimi ni kuhakisha kwamba ile standard ya production, ule ustawi wa zile vitu tunanunua zitainuka zaidi. Na hili jambo ni mhimu consumer rights tunataka kushtawisha consumer rights au haki za wateja ili kwamba tupate standards au ustawi bora zaidi ya vitu ambavyo tunavinunua na mambo kama hayo nilisema kwamba hatuna kwa njia inayofaa au inayopasa na kwa hivyo tumetoa muda fulani ili kanuni

ambayo instahili kufanywa kuhakisha jambo hilo kanuni hizo ziweze kuwekwa na Bunge.

Haki ya mshitakiwa, asiadhibiwe, ashidhalalishwe, tumepata mashtaka mengi mtu anashikwa njiani anaendelea na kazi zake huku atiwa kwenye cell, huko labda anapigwa, siku nyingine ni mgonjwa, siku tatu tunasikia mtu amekufa. So, mambo kama hayo lazima yasitahishwe na tumeweka haki ya mshtakiwa yeyote awekwe katika cell kwa njia iliyo nzuri, cell ambayo anaweza kulala huko, chakula apewe saa zile anangojea kuhukumiwa na saa ile ya kuhukumiwa anapelekwa kortini apewe haki pia ya kujitetea kwa njia yote. Akiwa hana wakiri hana pesa za kumuweka wakili basi Serikali impatie wakili. Tuna pia pendekezo pia kuweko public defender – mtetezi wa wananchi na ofisi yake itakuwa inashughulikia jambo kama hili la kuwatetea wananchi ambayo hawawezi kujitetea katika korti wakati wa kupelekwa kortini.

Kisha kama muonavyo sura ya tano ni ndevu kwa kuwa ni mhimu sana. Na ningependelea sana kila mmoja wenu aisome sura hiyo na aifahamu wazi wazi.

Sura ya sita inahusikana na mambo ya Bunge – representation of the people, uwakilishi wa watu, uwakilishi wa taifa au uwakilishi wa raia. Hapa tunazungumzia mambo ya elections. Uchaguzi wa kupiga kura tukasema kwamba uchaguzi utakuwa kwa secret ballot, ya siri sio ya mlolongo, tunasema kwamba elections zitahakikisha kwamba akina mama na walemavu na vikundi vidogo vidogo zile kabira ndogo ndogo mpaka sasa tumezidharau hizo kabila ndogo. Tumeziweka kando kusahau, tumekuwa tukishtaki kwa mfano kwamba hata katika ile list ya makabira iwemo inasemakana wao hawako nchini. Kwa hivyo tunasema watu hawa, walemavu, na akina mama, minorities wale wachache wachache pia wapate nafasi ya kushiliki katika maisha ya kijamii na hapa tunazungumzia maisha ya kisiasa, waingie katika Bunge au wao wawakilishwe katika Bunge kwa njia fulani.

Pia tunasema kuwe na kujiandikisha saa zote, muda wowote, kuwe na ofisi ya mtu kuwa kujiandikisha kuwa ni mpigaji kura kusiwe hali ilivyo kama sasa unangojea mpaka kuwe na tangazo kwa magazette kwamba mwezi fulani kwa muda wa wiki mbili au tatu kutakuwa na kujishalisha au kujiandikisha kwa wapiga kura. Kuwe na ofisi wakati wowote mtu akitaka kuenda kunjiandikisha aweze kujiandikisha wakati wowote. Pia tunasema kwamba… theluthi moja ya wagombeaji uchaguzi wawe ni akina mama. Kwa hivi sasa akina mama hawana sauti ya kutosha katika maeneno mengi ya umma, ya kijamii, ya kisiasa na kiuchumi. Hii ni njia ya kuhakikisha akina mama wana sauti angaa katika bunge au katika councils, baraza za mji n.k.

Pia tunasema kwamba kila chama cha kisiasa katika ile list yao ya ugombea uchaguzi waingize akina mama hapo. Pia ile list iseme kwamba iandikwe kwa njia ambayo akina mama watapita sio kuwa mama anatiwa mwishoni. List ya wanaume wote mwisho kuna mama mmoja, wawili, watatu. Iwe ni list alternative, unaanza na mwanamume, wapili atakuwa ni mwanamke, watatu mwanamume, wanne mwanamke n.k. ikiwezekana jambo kama hilo lifuatwe ili kwamba tupate akina mama wengi zaidi katika Bunge.

Pia tunazungumzia ni nani ambaye anaweza kujiandikisha kuwa mpigaji kura. Pia tunasema kwamba zile sanduku za kura ziwe transparent, unaweza kuona ndani kama kioo sio ya chuma ambayo huwezi kujua ndani kuna kitu ama hakuna kitu, unaiona ile kura yako ikiingia pale. Na kubakia pale. Na kuendelea mbele tunazungumzia viama vya kisiasa. Vyama hivyo vitaandikishwa na electoral commission, tume ya uchaguzi. Ili sasa vyama vya kisiasa nikiwa na chama changu nitaanziza nitaenda kwa Registrar of Societies mshajiri mwenye kuandikisha vyama vya kila aina. Kwa hivyo kazi hii ya vyama vya kisiasa sasa imepewa ile tume ya uchaguzi. Pia hiyo tume ya uchaguzi itashikiria kazi ya kusimamia uchaguzi wa kila chama. Kila chama si huwa na uchaguzi wake pia? Anawekwa mtu kwa Chairman, Treasurer, Secretary General n.k. Basi uchaguzi wa kila chama utasimamiwa na Electoral Commission ambayo inasimamia uchaguzi wetu hapa nchini ya kitaifa n.k.

Pia kila chama cha kisiasa kitaweka hesabu ya matumizi yake, ili kwamba tunjue pesa zinatoka wapi na zinatumiwa kwa njia gani. Ili wanachama wa chama kili wanjue kuwa pesa wanazotia kwa chama chao inatumiwa kwa njia inayofaa. Hazichezewi kwenye safari ya wale wakuu wenye chama kusafiri hapa na pale na kujitia petroli kwenye magari yao makubwa n.k. Ile idea ya transparency na accountability, ile mambo kufanya wazi na watu kufanyiwa hesabu pia iko katika vyama vya kisiasa. Viwe ni wazi wanachama wa kila chama wanjue pesa zao au pesa za pesa zao zinatumiwa namna gani.

Pia vyama vya kisiasa ambavyo vitaingia kwenye uchaguzi na kupata vote za kutosha zitasaidiwa na Serikali kwa pesa kuendesha kazi zao. Kutakuwa na funds, au sanduku maalum ya pesa ambayo italipa kila chama cha kisiasa pesa fulani kuendesha kazi zake, hasa kuendesha kazi zile za kuelemisha wananchi au wanachama wake juu ya demokrasia na juu ya haki za binadamu n.k. Ili kila mwanachama awe na maarifa juu ya haki zake na maarifa ya kutosha juu ya demokrasia ni kitu gani. Kwa njia hii tutainua hali na ushtawi wa demokrasia na pia hali ya haki za kibinadamu katika nchi yetu.

Tukiendelea mbele sasa tunasungumza juu ya Bunge na hapa tumefanya mabadiliko makubwa kidogo. Sasa tuna house national assembly, au la? National Assembly au Bunge. Sasa tumesema kwamba Bunge ambayo tunapendekeza kuwe na nyumba mbili. Kutakuwa na National Assembly kama tunayo hivi sasa, kisha kutakuwa na National Council. Pamoja hizi nyumba zitaitwa ni Parliament au Bunge. Hii ni system au mpango unatumiwa nchi kadha uraya, na kule America kwa mfano, two houses of Parliament. Waingereza kuna House of Commons, ambayo ni sawa na Bunge yetu ilivyo sasa watu waliochaguliwa na wananchi. Kisha kuna House of Lords, nyumba ya wahehe walio wakuu (Lords), inaitwa House of Lords maanake zamani Uingereza kabla ya miaka mia kadha Uingereza ilikuwa ikitawaliwa na watu wakubwa matajiri wenye mashamba makubwa makubwa; thousands and thousands of acres. Kwa hivyo democracy ilipoingia hapo wao walipewa nyumba yao. Kuna wale wamechaguliwa na raia wa apo wananchi, kuna wale hawakuchaguliwa lakini ni hao mabwana wakubwa. Lakini walitumiwa na hii system au mpango wao wa Ubunge, ikawa sasa kanuni inaundwa kwenye House of Commons inapelekwa House of Lords ili ichunguliwe zaidi. Na mara nyingi majadiliano katika House of Lords huisaidia House of Commons kusitawisha zaidi zile kanuni maana wanapata maoni mazuri. In other words House of Lords si mbaya hivyo, inayo faida yake.

Pia kule America utaona kuna nyumba mbili pia – kuna house of representatives na kuna senate mashehe – senate ingawa sio

zee kwa umri lakini inaitwa senators. Zote hizi pamoja zinaitwa Congress ndiyo the joint one. House of Representatives and Senate together forms Congress. Kwa hivyo tumefikiria kama hapa kwetu tunaweza kujaribu jambo kama hili kuwa na nyumba mbili mbili ambazo zitakuwa ni parliament moja. Na sheria inaweza kutungwa ama katika National Council au katika National Assembly. Na katika National Assembly, kutakuwa na Wabunge mia tatu. Mia mbili na kumi watakuwa ni hao sasa tunawachagua, sio? Kisha kutakuwa na tisini wengine. Watu wengine wametuambia hii ni hasara kuwa na nyumba mbili, ni hasala pia kuipanua hii National Assembly kuifanya mia tatu juu ya mia mbili na kumi. Tunasema sababu yake ni kwamba tunataka kushtawisha demokrasia katika nchi yetu. Maana kuna vote nyingi, kura nyingi ambazo zinapotea, kama kwamba mtu anazitupa kwenye mto au vichakani havitiwi kwenye hesabu na wale waliopiga kura hizo kwa hivyo hawana sauti katika Bunge. Kwa mfano, tuseme hapa Garsen kuna wagombea wachaguzi wawili kutokea. Moja akamshinda mwenzake kwa kura kumi tu au kura mbili, si inapatikana hivyo? Kwa kura mbili mtu anaingia kwenye Parliament, hiyo ni sawa. Lakini yule amepata kura kama hizo amefungua mbili tu. Kura zote zile huwa zimepotea, au sio? Kwa hivyo tunapendekeza sisi kwamba kila chama kura zake zote zile nchi nzima zitajumlishwa. Kila chama cha kisiasa kura zake zitajulishwa na kufuatia ile jumla ya kura zake zitapewa sehemu fulani kutoka viti hizi tisini zingine. Hii itakuwa kama reserve seats hivi na mtu anapewa kufuatia kura zake. Kwa hivyo kwa njia hii tunaona kwamba wale wananchi ambao kura zao hazikutiwa maanane pia zitafaidika kwenye hizo reserve seats tisini. Kwa hivyo vitaganywa kati ya vyama kufuatia jumla ya kura chama kile kimepata. Tunakubaliana hapo? Hii itastawisha demokrasia kila moja wetu atahisi kwamba ingawa mpiganaji kura niliotaka mimi hakupata lakini chama kile ambacho mimi napendelea kimepata viti kadha in addition zaidi. Hii ni system pia inatumiwa kule Uraya kwa mfano, kule Ugerumani inatumia system hii na inaitwa mixed member proportional system. Na tunasema kwamba nusu ya hawa hivi viti tisini, nusu yake viwe ni akina mama kutoka vyama tofauti tofauti. Sawa? Kwa njia hii tumepata faida kadha ya kushtawisha kidemokrasia na pia kuwapa akina mama sauti kubwa zaidi.

Hiyo ni National Assembly; kisha National Council ujumbe wake jumla watakuwa ni mia moja, hiyo nyumba ya pili. Na hawa watachaguliwa kutoka districts wilaya. Kila district kutapigwa kura si kuchaguliwa nominated au selected, elected. Watachaguliwa kwa kura wajumbe sabini kutoka kila wilaya Mjumbe mmoja au Mbunge mmoja. Viti thelathini vingine vitakuwa vya akina mama, akina mama wanne kutoka kila province tusema kama hapa Pwani watatoka kina wamama wanne. Pia watafanyiwa elections na watakuwa ni wajumbe wa coast province hawa wanne katika mikoa saba, 4 X 7 = 28, sawa? Wale wawili wengine kukamilisha kuwa thelathini watakuwa ni Nairobi kwa kuwa ni capital, mji mkubwa watapewa wanawake wawili kuwa Wajumbe wa Nairobi na Nairobi is also a province now. Sawa? Wote watakuwa ni thelathini kujumuisha na wale wabunge kutoka kila district watakua mia moja.

Pia kila nyumba National Council na National Assembly watakuwa na kazi zao. Kazi moja itakuwa ni hiyo moja wote wawili watatunga sheria Jumba hili la National Council litatunga sheria National Assembly watatunga sheria lakini National Assembly peke yake ndiyo ambayo itatunga sheria kuhusu budget, kuhusu matumishi ya pesa. Any finance bill mswaza wa kanuni unaohusu pesa utatungwa kwenye National Assembly. Otherwise, Bill ingine yeyote ile, sheria ingine yeyote inaweza kutungwa hapa na pale. Pia tumegawanya jukumu kati ya nyumba hizi mbili, National Assembly or National Council kwanza. National

Council ndiyo ambayo itakubali au kupitisha kukubaliwa kuwa na wanatume wengi sana. Kutakuwa na Tume kadha. Tume nyingine ni mpya nyingine ni hizo tunavyo sasa. Kwa mfano Judicial Service Commission, tume ambayo itachagua Ma-judge, Mahakimu. Wanachama wa Tume hiyo watachaguliwa lakini lazima National Council iwakubali. Inajukumu, au inamamlaka ya kukubali au kutokubali wanachama wa Tume itakayochagua Ma-judge.

Ethics and Integrity Commission hiyo ni Tume mpya hiyo Ethics and Integrity Commission. Hiyo ni Tume inahusika na kazi ya kuhakikisha kwamba kila mtu anaye mtumikia mwananchi ni mtu ambaye anatambia mzuri, ana jina nzuri, na pia ana mwendo mzuri. Ethics inakaribiana sana na ndini, ni mtu ambaye ana uaminifu unaweza kumtegemea, ni mwenye kusema ukweli ambaye anania safi ya kuendelesha kazi zake n.k. Kwa hivyo kutakuwa na Tume maalum ya daima kuhakikisha kwamba kila mfanyi kazi wa umma kutoka baraza la local govt. mpaka President mwenyewe, kuwa wote hao wanatumikia kwa njia nzuri. Hakuna ambaye ni haini hakuna ambaye anachezea mali ya umma, hakuna ambaye, ni mtu huwezi kuamini na chochote. Ethics and integrity.

Pia kutakuwa na National Land Commission, kwa hivyo wanatume wa hiyo integrity commission lazima wakubaliwe na National Council. Pia National Council ikubali National Land Commission, members of National Land Commission. Hii ni Commission ambayo itatunza na kufuatia mambo yote ambayo kuhusu ardhi na inafanyika kwenye mashamba na ardhi ya umma or ya taifa. Wanatume wake lazima wakubaliwe na National Council.

National Environmental Management Commission, Tume ya kutunza mambo ya mazingara. National Teachers Service Commission wanatume wa National Teachers Service Commission lazima wachaguliwe na kukubaliwa na National Council. Salaries and Remuneration Commission, Tume ya mishahara na malipo kwa wale wafanyi kazi, hiyo ni tume muhimu sana. Wanatume hawa lazima wakubaliwe wakishachaguliwa lazima National Council hiyo Bunge ya pili ambayo tumependekeza iweko, lazima wapitishe majina yao kwa kukubali, na hii ni Commission muhimu pia. Kila mfanyi kazi wa umma tangu Rais mpaka yule Messenger, katika ofisi ya Serikali, hii Commission ndiyo itakata shauri mashahara wake utakuwa ni ngapi. Mbunge pia mshahara wake utawekwa na hii tume inahusika na mishahara n.k. mtasoma wenyewe.

Kisha tuna Public Defender hapo, mtetezi wa umma, taifa yule ambaye ukiwa na shida umeshikwa umewekwa kwa gela watu wako wanamuendea ofisi kwake, ameshikwa mtu wetu hatuna pesa za kumuwekea wakiri tusaidie. Mtetezi wa taifa. Wote hawa appointment zao lazima zikubaliwe na National Council. Hiyo National Council tunayopendekeza iwekwe ina kazi zake za kufanya. National Assembly nayo pia kwa upande wake lazima i-approve uchaguzi wa watu. Prime Minister, Rais anamchagua Prime Minister lakini National Assembly lazima imkumbali. Isipo mkubali hawezi kushika kazi ya Prime Minister. Rais ajaribu tena amuchague mwingine na huyu pia jina lake lipelekwe National Assembly lazima imkubali huyo. Ikimkubali uzuri, ataunda Serikali yake, mawaziri wake kazi itaendelea. Ikiwa hakukubaliwa huyo wa pili pia aliyechaguliwa na Rais basi Parliament, Bunge, itavunjwa. Hiyo ndiyo hali moja tu peke yake ambapo Rais anaweza kuvunja Parliament. Ataivunja kwa kuwa Prime Minister aliyemchagua hakukubaliwa na National Assembly mara pili. Kwa hivyo sasa lazima uchaguzi mkuu mpya

ufanywe na Rais ajaribu tena. Yule ambaye atakuwa ni kiongozi wa chama chenye majority seats, Rais atajaribu tena kumchagua kuwa Prime Minister akipita uzuri mambo itaendelea. Kwa hivyo National Assembly ni muhimu katika ku-approve the appointments made by the President, the Prime Minister, Deputy Prime Ministers, Ministers, Deputy Ministers, Permanent Secretaries, Mabalozi, Electoral Commission, Auditor General- yule ambaye anafanya hesabu ya umma kuweka hesabu ya umma nzima au taifa nzima, Director of Central Bureau of Statistics, na Governor of Central Bank. National Assembly lazima ikubali watu hawa, ipitishe kwamba sawa huyu anaweza kushika kazi hii na anaweza kuendelea na kazi yake.

Sasa tunaendelea kuzungumzia sehemu nyingine inaitwa The Executive. Hii ndiyo mambo muhimu kuhusu Bunge ya jumba mbili tunafahamiana hapo sio? Sasa tunaendelea kufuatia The Executive. Serikali ina ghuso tatu, ina Legislature ambayo tumemaliza kuzungumzia sasa, Bunge, kisha Bunge inatunga sheria, sio? Sasa Executive Kazi yake ni kuendesha ile sheria to put it into operation. Na guso la tatu ni Judiciary – Ma-judge ambao wanakata shauri kweli hii sheria imetungwa na wenzetu kule Parliament lakini inaendeshwa kwa uzuri au haiendeshwi kwa uzuri, inapelekwa kortini, sio? Kwa hivyo guso hizo ndizo guso tatu za Serikali.

Sasa tunaingilia hii guso la pili The Executive. Na hapa tunasema kwamba mtaona kwenye page kuna picha wale wenye copy tunasema kwamba Structure of the National Executive, the National Executive in the Republic of Kenya, comprises the President, Rais, naibu wa Rais na Cabinet, baraza la mawaziri. Hao ndiyo pamoja wanauda Executive. Kisha tunaeleza mamlaka ya Rais or jukumu zake. Tunasema kwamba Rais atakuwa ndiye kichwa cha dollar, kiongozi wa nchi au Head of the State, atakuwa ni mkuu wa majeshi ya Kenya – Commander-in-Chief of Defence Forces, hatusemi Armed forces tunasema Defense forces tumebadilisha jina hapo. Defense Forces ndiyo bora kuliko Armed Forces, tunaona kisha tunasema Rais atakuwa mwenyekiti wa National Security Council, Baraza ya Amani ya Taifa.

Pia kutakuwa na baraza lingine, Rais atakuwa ni mwenyekiti wa Defense Council, baraza ya ulinzi – kuna baraza ya amani na baraza ya ulinzi na kila baraza kazi zake mtaziona hapa zimeandikwa. Pia tunasema Rais atakuwa ni ishara, kinara cha umoja wetu, ukimuona yeye unajua yeye ndiye kinara wa umoja wa taifa pia atakuwa na madaraka au kazi ya kuendesha na kushtawisha umoja wa taifa letu, ata linda ufalme wetu sio lazima afanane na crown, la. Ufalme wetu uweze kujiendesha au kuendesha serikali yetu tunavyopenda sisi kuingiliwa na mtu yeyote. Hiyo ndiyo sovereignty, kwa Rais ndiye atakuwa na jukumu ya kulinda our sovereignity. Na pia ataendesha mbele na kuheshimu hali yetu tukiwa makabira tofauti tofauti na watu wa dini tofauti tofauti na wa lugha tofauti tofauti. Lakini atahakikisha kwamba sote, lugha zetu na utamaduni wetu unalindwa na yeye ndio atakayetusomea na kutulinda. Na pia atalinda haki za kibinadamu katika nchi zetu na uhuru wetu wa kila aina kama nilivyoeleza uhuru wa kila aina sio? Uhuru wa kusema, uhuru wa kidini uhuru wa hivi na vile n.k. Hii ndio mamlaka ya Rais.

Na pia tunasema kwamba Rais asiwe na kazi yoyote nyingine isipokuwa hizi. Kwa hivyo rais hawazi kuwa mwanachama wa chama chochote. Mwanzo saa ile akichaguliwa atakuwa ni mwanachama wa chama fulani cha kisiasa. Lakini akishaingia kwa Rais atajiepusha na chama chile ili kwamba abakie neutral maanake sasa yeye si Rais wa chama fulani ni Rais wetu raia

anatusemea sisi wote hapendelei chama hiki au chama kile. Ametoka chama kile lakini sasa amechaguliwa amekuwa above all parties juu ya kila chama cha kisiasa. Hiyo ni kuhakikisha kwamba atakuwa mwaminifu kuwazingatia watu wote.

Pia tunasema Rais ataifungua Parliament, Rais ataita Parliament kuzungumzia jambo lote muhimu wote akitaka kuwaita he is going to special seat n.k. Rais ndiye pia atakayechagua baraza la mawaziri kumwanzia Prime Minister lakini baraza hilo lazima likubaliwe na National Assembly, majina ya mawaziri hao na Prime Minister yapelekwe kama nilivyoeleza. National Assembly wapitishe majina hao.

Ni nani ambaye anaweza kuwa Rais? Rais lazima awe ni mwananchi, amezaliwa in Kenya awe kati ya miaka thelathini na tano na sabini asiwe mdogo zaidi ya thelathini na tano asiwe mkubwa wa miaka sabini. Lakini pahala pengine tumetaja kwamba sharti hii ya umri haitahusikana na uchaguzi utakayofanyika sasa – ujao huu. Hapo mtu wa umri wowote anaweza kuingia. Kuna wengine wanatuambia mmeweka sharti hii ili kumnyima fulani nafasi ya kupata Rais kwa hivyo tunasema hii ni transitional thing. Ni ya kimbele kidogo. Pia tunasema kwamba awe na tabia jema asiwe na aibu yeyote mtu huyo ambaye atakuwa Rais, asiwe na doa lolote, asiwe na aibu yoyote. Awe pia na shahada ya degree kutoka university au chuo kikuu kinachojulikana na pia amepelekwa mbele na chama cha kisiasa. Pia anaweza kuwa independent. Mimi simo, au yeyoto kati yetu – I don't belong to any party pia anaweza kusimama kuwa Rais. He is nominated as a registered candidate by at least 1000 registered voters, akipata wananchi elfu moja kumpa recommendation, naweza kupeleka jina langu pia nikaomba nipigiwe kura niwe Rais. Sawa? Tumefungua kwa hiyo mlango kwa kugombea kiti cha Rais kwa mwananchi wa ada ambaye anafikiri anaweza kutumikia nchi yake.

Pia tunazungumzia jinsi ambavyo Rais anaweza kuondolea katika hali fulani… mtangoja kidogo ile Gladys pale-- Tuendelee mbele. Nilikuwa nasema Rais anaweza kuondoshwa kwenye kiti chake katika hali fulani. Hali moja ni ikiwa ni mgonjwa, kimwili au kiakili, na kuna wale ambao wanafikiri hawezi kuendesha kazi yake. Ikiwa nusu ya wanachama au wabunge wa National Assembly wanasema Rais hawezi kufanya hii kazi maana ana ugonjwa huu au ule basi kutafanywa kamati ya madaktari watano watakaochunguza ikiwa ni kweli Rais ni mgonjwa kiwili au kiakili. Akiwa atadhibitika kwamba kweli ni mgonjwa hawezi kuendesha ile kazi Rais ataondolewa. Lakini ikiwa hawa madaktari watasema la, anaweza kuendelea na kazi yake "we as doctors certify that he can continue", ataendelea na kazi yake. Hiyo ni hali moja.

Pia hali nyingine hii National Assembly, unajua kuna majumba mawili tumependekeza, National Assembly itakata shauri juu ya hali ya afya ya Rais. National Council pia inauwezo kama huo lakini ni tofauti kidogo. National council ikiwa kutatokea, theluthi mbili ya National Assembly again wanasema Rais amevunja Katiba, au amefanya mambo mambaya sana – gross misconduct basi ikiwa theluthi mbili ya National Assembly watapitisha motion kwamba the President is guilty of gross misconduct or the President is guilty of the bleach of the constitution, amevunja sheria hii kubwa ya katiba. Mkiwa theluthi mbili ya wanachama wanasema hivyo, basi pia kutafanywa uchunguzi kweli au si kweli. Na uchunguzi huo utafanywa na National Council, watasema National Council ndiyo walipitisha kwa hivyo pelekeni National Council sasa ifanywe uchunguzi. National

Council itaweka kamati kuchunguza jambo kama hili. Pia ikidhibitika ataondolewa, isipodhibitika Rais atabaki kwenye kiti chake.

Kisha twazungumzia jinsi ambavyo Prime Minister atachaguliwa baadaya ya siku saba ya uchaguzi yule mkubwa au kiongozi wa chama kilicho pata kura nyingi baada ya siku saba za elections ataambiwa na Rais atamwita, sasa wewe mimi nakuchagua wewe uwe Prime Minister na atapelekwa mbele ya National Assembly. Ikipitisha sawa, isipopitisha anapelekwa mwingine, asipopitishwa basi bunge itavunjwa na uchaguzi mwingine utafanywa. Huyu Prime Minister akipitishwa atachagua mawaziri wake. Yeye ni Mbunge, Prime Minister lakini waziri wake na wasaidizi wa waziri wake lazima wachaguliwe kutoka nje, lakini akileta majina yao lazima ya apitishwe na Bunge. Akichagua marafiki wake au jamaa wake, asema hawa ndiyo mawaziri wangu. Lazima Parliament itazame huyu anauwezo gani, amesomea wapi, ana experience gani, kweli afaa au hafai. Afaa apitishwe Huyu mwingine afaa, hafai, huyu afaa huyu afai, wale ambao hawakufaulu lazima Prime Minister achague wengine mpaka wote wapitishwe hawa ndiyo mawaziri wa Serikali mpya. Na kiongozi wa Serikali hiyo atakuwa ni Prime Minister. Mtapata maelezo mkisoma zaidi hapo. Kisha tunaingilia Judicial, guso la tatu.

Judicial and legal systems: Mahakama, Ma-judge, na hapa badiliko moja liloko ni kwamba tulikata shauri kwamba kuweko na korti kubwa zaidi ambayo inaitwa Supreme Court. Hivi sasa hatuna korti hiyo. Na tunaona kwamba kuna mambo fulani ambayo ni bora kuwe na korti ya appeal kushughulikia mambo kama hayo na mkubwa wa korti hiyo atakuwa ni Chief Justice, Mkuu wa Ma-judge. Na pia mabadiliko mengine ambayo yatakayofikiriwa zaidi ni Waiislamu. Tumesema kwamba korti za ma-kadhi zidhibitishwe hesabu yake. Kutakuwa na korti za Kadhi thelathini, chache kabisa ziwe thelathini. Hivi ni kuhakikisha Muislamu na mambo yake ya raia Muislamu na mambo yake kuhusu ndoa, talaka, ulafi anapata huduma ya utumishi kwa kadhi karibu na yeye, ili sasa mtu anakwenda safari ndefu kabla kumfikia Kadhi. Kwa hivyo theluthi Kadhi courts at least will be constituted. Kisha pia tunasema ni nani anaweza kuwa Kadhi. Kadhi lazima awe mwanasheria, ambaye amesoma akapata degree au shahada kutoka university awe ni kama wakili ambaye ametoka university leo. Ili makadhi wetu wawe ni makadhi wa aina …. na atakuwa amepata shahada katika elimu ya sheria za kiislamu. Kwa hivyo hatutaki kumuchukua mtu kutoka madrasa fulani hapa, katika mtaa fulani ule tukamuweka tukamwambia huyu ni Kadhi sasa. Twataka mtu ambaye ana ujuzi wa sheria awe Kadhi. Chief Kadhi pia lazima awe ni mtu ambaye ni Muislamu umri wake usipungua miaka thelathini na tano, awe pia ni mwanasheria, amesomea sheria ya Kiislamu katika University na ana experience miaka kumi. Kadhi awe na experience ya miaka mitano lakini Chief Kadhi lazima awe na experience ya miaka kumi. Pia kwa heshima zaidi yule Chief Kadhi atakuwa ni mwanachama katika ile commission, ama ile tume ya kuchagua mahakimu. Yeye atakuwa ni member, Judicial Service Commission. Pia kutakuwa na mwanamke wa Kiislamu atakayechaguliwa na vyama vya Kiislamu ama chama kikubwa cha kiislamu hapa nchini, pia awe member katika tume hii. Kwa hivyo kwa njia hii tumefanya mabadiliko hayo katika hii system au mpango wa sheria katika nchi yetu.

Natukiendelea mbele kidogo tunafikia mwisho, samahani, ni muhimu kuwaeleza nafikiri, natumae hamukuchoka sana lakini muhimu mambo yaelezwe vizuri ili tupunguze baadaye maswala mengi. Kwa hivyo hatutapoteza wakati ikiwa tutapunguza pia

maswala.

Na sura la kumi ni mhimu pia, muhimu sana. Inaitwa devolution of powers, mgawanyo wa mamlaka. Mamlaka ni kila kitu katika nchi, sio? Tumepata malalamiko mengi kwamba mamlaka yametiwa katika mikono ya watu wachache. Kwamba kuna haja mamlaka yaeneshwe kidogo kwa masilahi ya wananchi na kwa masihali ya nchi yenyewe. Pia umuhimu wake ni kwamba italeta ugawanyo wa mamlaka ipeleke huduma pia za watumishi wa serikali karibu zaidi na mwananchi. Na wananchi katika hapa mashinani watapata nafasi kushiliki katika jinsi ambavyo wanatawaliwa. Twaona hii ni njia nzuri ya kugawanya. Kwa hivyo tumeaanza mashinani kabisa. Tumesema kwamba katika kila kijiji kutakuwa na baraza ya kijiji – village councils na wazee wa kile kijiji ndiyo watapewa kuwa wana chama. Wazee hao ama watachuguliwa kwa kura au kukiwa kijiji kile wametosheka na wale wazee wao – elders hawa watakuwa ndiyo wataunda baraza ya kijiji na baraza hiyo itazungumzia mambo yanoyohusu ile kijiji, malalamiko yao, mapendeleo yao na kadhalika. Na kisha kila kijiji kitapeleka mjumbe katika council ya pili kwenye location, kutoka kijiji tunakwenda location. Kwenye location kutakuweko wajumbe wa vijiji. Kwa hivyo hao wajumbe wa vijiji wataunda baraza la location. Kila kijiji kitapeleka wajumbe wawili kwenye location councils. Na hapo pia watazungumzia hali ya localtion yao mambo ambayo yamekwenda kombo pale vipi kustawisha mambo hayo na kadhalika.

Na kila location bila shaka itakuwa ni sehemu ya wilaya. Sehemu ya wilaya pia itakuwa na Serikali yake District Government. District Government itakuwa ni elected government. Watu watapigania viti kwenye district council, kuunda Serikali ya wilaya. Jamaa wengi hapa na pale wamesema wanataka majimbo, sisi tumefikiria kwamba tukileta utumishi kwa raia karibu zaidi kwa jimbo ni bora kuliko to give powers to the region. Give powers to the district. Kwa hivyo tumesema kuwe na serikali ya wilaya. Katika Serikali hii ya Wilaya kutakuwa na council au baraza. Wanachama wa baraza hiyo watachaguliwa na wananchi wenyewe watagombea viti vya council. Mkuu wa council hii ataitwa District Administrator. Na council hiyo, itapewa mamlaka kuendesha mambo katika wilaya hiyo kufikilia mashinani na huduma zote ambazo mwananchi atazihitaji yeyote kati yetu. Kila district council itapewa uwezo kuendesha kutoa utumishi huyo kwa kila mwananchi.

Wale ambao wananakala au copies sijui wangapi, wawili watatu hapa, katika page 45 mtaona list. Sasa tumegawanya mamlaka kati ya Serikali mbili, Serikali ya kati ya Nairobi – Central Govt. na Serikali ya Wilaya. Wengine walitaka tugawanye kati ya Serikali ya kati na Serikali ya Jimbo. Sisi tumeona ni bora kugawanya mamlaka kati ya Serikali ya kati Nairobi, na District. Serikali ya kati itashughulikia mambo inayohusu, ulinsi wa nchi, amani ya nchi, mambo inayohusu mahusiano kati ya Kenya na nchi zingine - international relations, mambo inayohusu telecommunications – mawasiliano ya kisimu na kadhalika. National resources, mali ya kiasili ya nchi, National elections – uchaguzi wa nchi nzima, formation of national policy – kuweka mpango wa siasa ya nchi, currency au pesa, lazima pesa zichungwe na Serikali ya kati sio? Mahakama au korti, citizenship - mambo ya uwananchi, uraia, National public service, utumishi wa Serikali, Public Service na kadhalika. Pia mambo inayohusu Central Bank au Banki ya Kati, na kadhalika hii ndiyo imeachiwa mamlaka ya Serikali ya Kati, Nairobi.

Serikali ya kila wilaya, tumetia list ya pili hapo, District Government, list mwisho kabisa wa page 45 mmeshapata? Mstali wa

mwisho kabisa. Hapa tunaeleza jukumu au mamlaka ya Serikali ya wilaya. Katika eneo ndogo hilo Serikali za wilaya itakusanya kodi tofauti tofauti local taxes, kodi za hapo hapo kwa mfano kodi ya ushuru, kodi ya soko, na kadhalika. Kisha watatumia matumishi hayo au pesa hizo za kodi zilizokusanywa hapo pamoja na mswaada wa kutoka Nairobi na kila District itasaidiwa na pesa pia na Serikali ya kati itatumiwa kutoa huduma, utumishi kwa wananchi. Utumishi wa aina gani? Itatoa utumishi wa elimu, elimu ya primary na elimu ya secondary. Elimu ya pre-primary, ya nursery itatolewa na serikali ya wilaya.

Pia medical na health services, matibabu hiyo itakuwa ni mamlaka ya serikali ya wilaya tu. Huduma ya maji, kuhakikisha kwamba wananchi wana maji itakuwa ni jukumu ya district council. Market and trading centers viwanja vya biashara au soko n.k. District planning kufanya mpango wa kustawisha district kwa njia bali bali hapa kutafanywa skuli, hapa kutakuwa na clinic pale kutakuwa na uanja wa kuchezea wananchi, hapa kutakuwa na stadium, na kadhalika.

Pia utumishi kwa wakulima, agricultural services zitolewe hapo hapo, social rehabilitation, tusema kama shida ya street children shida ya watoto wanaozurura hawana kazi ni waajibu wa Serikali ya district kuhakisha kwamba mpango unafanywa kusaidia watoto ama uzee wao wapatikane walishwe nyumbani au wa wawekee kituo chao cha kukalia na kadhalika. Cultural affairs, mambo ya utamaduni, kila district inautamaduni wake wa kiasiri, mambo inayohusu utamaduni wa ile district itasimamiwa na district council. Kwa hivyo naona kwamba district council italipa mamulaka mengi sana. Na wengine watasema district nyingine hazina na pesa za kutosha hatuwezi kutoa utumishi wote huu kwa mapato tutakayopata kule.

Tunasema kwamba mali ya sili, ya umma, ingawa Serikali itakuwa yenye kupokea, kusimamia, Serikali italazimishwa na katiba hii kwa njia tofauti kuipa kila District Council pesa kiasi fulani. Kiasi hicho cha pesa, ya kupewa kila district au kila wilaya itategemea vitu viwili; ile population ya ile district na Geography yake na mapato yake ya kiasili pale pale. Wilaya ambayo haina mapato mengi semi jagwa, kuna labda kidogo mifugo na kadhalika haina kilimo, haina mapato ya utalii, haina forest ambapo mtu anaweza kupata kitu, akakata miti akauza mbao na kadhalika basi Serikali itaipa District hiyo zaidi kuliko tuseme kama District ya Mombasa ambayo inamapato kutoka bandari pale, mapato ya utalii na kadhalika.

Pia tunasema, kwamba lile eneo kuna mali ya sili – natural resources, eneo lile lazima sehemu fulani au percentage fulani ya mapato yanayotoka kwenye mali hiyo ya akisiri lazima yatumiwe pale pale katika ile district. Na kama hapo ni eneo ya utalii percentage fulani ya mapato ya utalii lazima ibakie hapa. Au kuna madini fulani hapo imepatikana kama kule kwale kumepatikana madini, sio? Sehemu fulani ya hiyo mapato ya madini lazima itumiwe pale pale. Juu ya mapato mengine kutoka uvumbi, kutoka tuseme utalii na kadhalika.

Kwa hivyo ikiwa mpango huu utafuatwa bila shaka kila district itaweza kupata income ya kutosha kuwapa wananchi kutoka district ile utumishi ambao watatumia, elimu, matibabu na kadhalika. Nafikiri ni hayo tu, ambayo ningependa kuyasema kuna mengi mengine lakini afadhali aniwachie hapo, tumekaribia saa saba. Tumesema kwamba tuna tume kadha sitakazoundwa, tume ambazo zina kazi muhimu sana moja kwa mfano itakuwa ni tume ya Human Rights and the Adminstration of Justice, pia ni muhimu sana kwa haki za binadamu. Mtu akiwa na lalamiko lolote haki zake zimeingiliwa kuna njia yakupata haki hizo. Kuna

eneo fulani anapata haki ya kustawishwa kwa njia ya kutosha. Kuna council inaitwa Economic and Social Council. Hiyo kazi yake, council hiyo au baraza hilo ni kutazama kila eneo la Kenya kupeleleza mambo inayofanyika pale, hiyo maendeleo ni sawa au si sawa, area hiyo inapata haki yake au haipati haki yake na itafanya mabadiriko ya kutosha. Commission hiyo hiyo, au baraza hilo hilo la uchumi na kijamii ndilo baraza inayoshugulikia mambo ya investment kuhakikisha ambao wale ambao wako na rasilimali wanaweza kuja hapa na kufanya mipango mizuri ili kwamba mtu aje na pesa zake za nje na kutia pesa zake pale.

Samahani nimesema nitasimama hapo lakini nimeacha jambo moja muhimu sana lazima nilitaje nalo ni kuhusu ardhi. Ardhi ni muhimu sana, itachukua muda mfupi tu kueleza. Tumesema ardhi ni musingi wa maendeleo katika Kenya. Land being Kenya's primary resource ndiyo mali ya kiasili kubwa kabisa katika nchi na ardhi ndiyo musingi wa maisha kwa watu wengi hapa Kenya. Tunasema kwamba lazima hali yake istahilishwe na tumependekeza mambo matatu nanne hapa, katika eneo hili la ardhi. Tumeipa kufuatia mswaada huu, tumeipa Serikali miaka miwili kufanya mabadiliko na kustawisha mambo yanayohusu ardhi. Tunasema katika muda huo wa miaka miwili baada ya katiba hii kupitishwa kwa njia iliyo rasmi, bunge itapitisha sheria kustawisha kanuni zote zinazohusika na ardhi hapa nchini. Tumeambiwa na watu wengi sana na wanamaarifa juu ya mambo haya, kwamba sheria zetu zinazohusu ardhi ni nyingi zimetapakaa hapa na pale kuna haja ya kuzikusanya na kurekebisha na kustawisha ili ziwe zafahamika kwa njia iliyo bora zaidi. Na tukasema kwamba kuwekwe ushtawishi au system na pia siasa ambayo itawezesha serikali kusuruhisha kila ungovi unaohusika na ardhi. Tuna lots of land disputes. Sio? Kuna ugovi mwingi hapa na pale. Kwa hivyo twasema kwa muda wa miaka hiyo miwili serikali itafute tasisi au njia za kuhurutisha ungovi uliyoko katika eneo hili la ardhi.

Pia tunasema katika muda huo huo wa miaka miwili wale wanaoitwa masquata, au wasio na ardhi au mashamba wapatiwe makao. Tusiwe na squatter baada ya miaka miwili katiba hii katiba kupitishwa. Pia tunasema katika muda huo wa miaka miwili Serikali itafanya uchunguzi katika mashamba na ardhi zilizotolewa miaka hii yote ili kuhakikisha ikiwa mashamba hayo imetolewa kwa njia iliyo sawa. Na ikiwa imetolewa kwa njia isiyo sawa basi itachukuliwa na Serikali na kupewa wale ambao wanahaja na ardhi hizo kwa njia iliyo halali. Haya ndiyo mapendekezo yetu.

Pia tunasema kwamba hasa katika muda huo wa miaka miwili kutawekwa njia ya kuchugua na kupata makisio ya malalamiko tujue malalamiko hayo ni makubwa, madogo ni hatari ama vipi. Ukubwa wake na uzito wake na umuhimu wa malalamiko hayo katika maeneo fulani hasa, katika North East, katika Coast na katika Rift Valley. Katika mikoa hii mitatu ndiko ambako shida ya ardhi ni makubwa zaidi. Kwa hivyo tunaomba serikali katika muda wa miaka miwili baada ya hii katiba kupitishwa ichungulie malalamiko yaliyoko hapo na kutafuta njia ya kuyatatua. Haya ndiyo mapendekezo yaliyoko. Tumeeleza hapo aina tofauti za ardhi; kuna trust land, kuna govt. land, ambayo tunaita public land na kuna private land ile ambayo iko katika mikono ya watu binafsi. Na nifikiri kwa hapo na baada ya muda usiopungua masaa mawili bila shaka mmechoka kunisikiza na sasa kwa muda wa saa moja tu, tutasikiza maoni yenu juu yale niliyoeleza, mtanieleza ikiwa jambo nimelisema hamjafahamu, mwataka nirudie na njia ambayo tutaifuata mtainua mkono, tuhesabu kila mtu tutampa number yake na tutafuatia mpango huu number 1, ataanza yeye number two, n.k. Asanteni sana kwa kunisikiza na nitamuachia District Coordinator sa kutuongoza

katika kuuliza na kutoa maoni yenu. Asanteni sana. (clapping)

**District Coordinator:** Asante sana na pongezi Com. Salim kwa sababu umeangalia Katiba ambayo ni refu lakini umejaribu kuzungumza yale ambayo ni muhimu sana kutokea mwanzo kufika mwisho nafikiri tumeelewa. Sasa kama vile ambavyo amenipa wakati huu kuongoza kipindi cha maswali. Ukitaka kuuliza swali au kutoa maoni yako inua mkono; na nafikiri alisema kwamba tutaanza, yaani ili tuweze kuwa systematic tutaanza mwanzo kama unajambo vitabu munazo tumezitoa lakini inaonekana wengine labda hamkuja nazo lakini tumezigawanya vingi sana. Tulikuwa na mkutano hapa vingine tulipeleka mpaka mjini vingine tukapeleka Tarisa na sehemu hizi zote. Garsen ni kubwa lakini inaonekana leo labda hamkuja nazo lakini si neno, zile za kale ambazo ziko tutaangalia, ya kwanza, ya pili ya tatu, ili tumalize haraka. Tutaanza na upande huu, maanake nimeona mkono wa wakiri umekuwa wa mwanzo ndiyo nikasema one, ningependelea tuanze na number one hapa. Utasema jina halafu utasema yako.

**Danson Buya:** Jina langu ni Danson Buya Katana. Habari yenu? Mimi ni mmoja wa wale District delegates ambao tumechaguliwa kupitia elections ilifanywa na councillors juzi kwa ajili ya national conference. Jambo la kwanza ambalo ningependa Prof. aliangalie wakirudi Nairobi na ambalo linasumbua watu wengi Tana River ni Affirmative Action. Yaani District yetu, imebaki nyuma kwa njia nyingi sana kutoka Bura mpaka Kipini. Constitution au Katiba mpya ambayo inakuja itafanya nini au imeweka jambo gani kuweza kutusaidia na sisi ambao tuko nyuma kuweza ku-catch up na watu wengine. Hiyo point tulisema hapa wakati walikuja kwa maoni tulisema katika Kipini wakati walikuja kuchukua maoni lakini hiyo point katika constitution mpya mimi sijatosheka kama mkaazi wa Tana river kwamba katiba mpya imetoa pendekezo gani ya kuwa itatuwezesha sisi kwa mfano tupate mashule na tupate hospitali za kutosha?

Pendekezo langu ambalo tumelisema siku ingine hapa ni kwamba katika miaka mitano wakati katiba mpya itakuwa imepitishwa tuwekewe senti za kutosha kwa watu wa Tana River District. Ya kwamba na sisi tuweze kuletwa mbele, maanake tukisema tutakuwa pamoja tunaanza maisha mapya lakini wewe uko nyuma wale wako mbele wataendelea na sisi tutabaki pale pale nyuma. Kwa hivyo hiyo pendekezo ninaomba Commission iangalie sana katika mipango yake itakayokuwa.

Kitu kingine ni kuwa Commission haijatuelezea kwa kinaganaga kwamba ni sawa na tunawapa pongezi kwa sababu ya hizi Serikali za kawaida ambazo tutakuwa nazo hapa. Ni vizuri sana lakini kule kwa national, kwa ma-commission na zile ofisi kubwa kubwa kwa mfano, mtu wa Tana River tuna uhakikisho gani ya kwamba wazaliwa wa Tana River ambao watakuwa National Environmental Management Committee kwa mfano mtu wa Tana River, na yeye atakuwa katika Public Service Commission kwa mfano, mtu wa Tana River na yeye atakuwa kwa hiyo Land Commission, kwa mfano, mtu wa Tana River na yeye atakuwa katika hiyo Social Ethics Commission ambayo itachaguliwa. Tunasema sisi watu wa Tana River kwa muda mrefu tumepitwa na mambo mengi na hatutaki tena katiba hii mpya itupite tena. Kwa hivyo tunaomba hiyo point iangaliwe na sisi pia katika hali ya kazi kubwa kubwa, kama kazi ya Ambassader, kazi ya Permanent Secretary na kazi kama hiyo, mtu wa Tana River ako na nafasi gani katika hiyo Serikali mpya ambayo Kenya inataka kuweka kupitia kwa katiba mpya.

Point nyingine ambayo ningependa Commission wakiondoka hapa wakaifikirie ni kuhusu utumishi wa senti za umma yaani public expenditure. Mtu wa Tana River akienda kununua soda, na yeye anapatiwa senti, anapeleka tax ile ile kiwango mtu wa Nairobi na mtu wa Mombasa anapelekewa. Lakini katiba mpya haijasema kwamba ni pesa ngapi ambayo itakuja Garsen kwa mfano, Constituency ya Garsen, Constituency ya Galore, Constituency ya Bura, tunasema ikiwa Kenya kwa mwaka huu imepata billion ishirini na nne, tunataka waziri wa fedha ikiwa anasimama kusema kwamba ni pesa gani amepokea na nipesa gani atatumia atuambie hapa Tana River District ni centi ngapi zitakuwa zikitumika kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Tana River District. Hii point tunataka iangaliwe sana. Kwa sababu kwa katika Katiba ya sasa nafikiri kifungu cha mia moja na kumi au mia moja na moja, inasema kuwa waziri wa finance atasimama na atatoa musimamo wake zile centi amepokea na zile centi atatumia. Lakini katiba haielezi atapeleka centi ngapi kwa district fulani. Sisi tunataka watu wa Tana River tufanye direct benefit. ikiwa ni 24 billion imepatikana wagawanye na sisi watu wa Tana River tupate fraction yetu na sisi tuweze kuendelea. Kwa hivyo katika hali ya public expenditure, na ile collection ya pesa, tunataka katiba mpya iangalie hii maneno na tuweze kupatiwa nafasi yetu specific.

Kitu kingine cha mwisho, na nikiwa ninakaa maanake wengine wataendelea. Mara nyingi tunasikia Serikali imeenda imechukua misaada na tunasikia pengine Kenya wewe mtu wa Tana River unandaiwa shilling million ngapi, wewe hukuenda kuchukua hiyo pesa, public debt. Haukuenda kuchukuwa hiyo pesa hatukuambiwa ni pesa ngapi tunachukua kwa IMF au kutoka kwa World Bank au mahali fulani, lakini sisi na sisi tutabeba hiyo problem na watoto wetu tukija kuwazaa tutabeba hiyo maloan ambayo tunabebana nayo. Pendekezo liloko ni kuwa katika katiba mpya ambayo inakuja tunaomba kwamba na sisi sauti yetu kama wananachi isikizwe tuambiwe ni pesa ngapi kabla ya Rais au waziri wa fedha kuenda kutupatia madeni. Atuambie anaenda kuchukua deni kwa pesa ngapi, atalipa interest ngapi, na tujue sisi watu wa Tana River tunabenefit kwa namna gani. Kwa sababu vile inafanyika siku hizi unasikia tu kumeandikwa agreement, Serikali imechukua madeni sisi hatujui tumepata benefit gani na sasa Serikali ina mandeni mengi lakini hatujui kama hapa Garsen madeni hayo ni ya nini na sisi tume-benefit namna gani. Kwa hivyo issue hiyo ya public debt tunaomba sana katika katiba mpya waziri asiwe na nafasi ya kuchukua pesa kutuingiza kwa madeni kama sisi wananchi hatujapewa nafasi ya kuzungumza. Na isiwe tu kuwa ni Bunge au ni hao masenators, tunataka wananchi wenyewe wapewe taarifa kamili ili sisi tujue kwamba Serikali yetu inaenda kuchukua pesa namna hii na mtu ata-sense ata-benefit namna gani kutokana na hizo senti. Nawashukuru na wenzangu wengine watachangia mengine mengi, asante sana bwana Coordinator. Thankyou.

**District Coordinator:** Sasa napendekeza kwamba ukisema jina lako jaribu swali lako liwe fupi kwa sababu tuna muda mfupi. Mwenzangu alinisaidia alitoa karatasi hapa tuna watu kumi na kila na moja ambaye ameinua mkono anataka kuzungumza. Kwa hivyo wewe ni wakwanza. Wa pili? Njoo mbele tafadhali, sauti yako lazima iingie hapo.

**Hussein Kiribaye:** Mimi kwa jina naitwa Hussein Kiribaye. Nilikuwa na maswali mawili ambayo kulingana na hiyo draft, nimeona kidogo kuna sehemu mbili ambazo nilipoziangalia nikaona kidogo ziko open sana. Chapter 4 verse 17 (A) ambayo

inazungumzia kuhusu citizenship. Kulingana na vile ulivyo zungumza, ni kwamba hii draft ikija inforce mtu yeyote ambaye ataonekana, ama atakuwa hapa kwa nchi ni mwananchi. When the Constitution comes into force huyu mtu atakuwa ni mwananchi. Sasa swali langu ni kwamba mtu hua, ardhi haikui ikiwa hiki kipengele kitaachwa open hivi na saa hivi watu waje ile itakuwa enforced ni draft lakini waachwe na waingie Kenya, kabla ya hii ikuwe enforced lakini ikiwa enforced wawe wako hapa (interjection: (inaudible) Chapter 4: 17 one, (interjection: Com. Salim; (inaudible) maanake nilikuwa naona kama kipengele cha kwanza wakiingia baadaye constitution ikiwa in force watu watakuwa wengi ardhi itakuwa kidogo.

Sehemu ya pili ni kwamba funding ya hizi parties. Kuna kipengere cha kwamba the State will fund the parties ambazo zitakuwa sure. Sisi tunategemea hizi resources zetu, ikiwa Kenya watatengeneza vyama mia mbili, hiyo pesa ya ku-fund hizo parties tu tatoa wapi? Maoni yetu ni kwamba ikiwa watu watatengeneza chama wajipange wenyewe hatuna pesa ya kuwapatia watu ambao wanatengeneza vyama mia moja au mia mbili.

Sehemu ya tatu, President atapigania u-president wakati ako na chama fulani, kulingana na hii draft, akipata u-president anatoka kwa chama halafu hatategemea, tutakuwa na uhakika gani, kwamba hatategemea kile chama ambacho alikuwa ameenda nacho kwa Bunge? Definitely kutakuwa na favouritism ndani ndani ambacho hicho clause kimachwa open. Kwa hivyo kama kuna njia ingine, iweko lakini akipigania na kile chama chake, halafu akipita lazima atategemea atalalia upande, asante. (clapping).

**District Coordinator:** Asante sana, sasa watatu, yule watatu ambaye yuko hapa. Haya kama huko tayari yuko wa nne? Haya wa nne. Watatu kama umesahau utakuja baadaye.

**Mureithi Pius:** Asante kwa majina naitwa Mureithi Pius nafanya kazi Malindi. Lakini nina maswali mawili, la kwanza ni mambo ya structure ya Government, kwa sababu mmesema Government itakuwa, na devolution of powers. So the problem is the structure is very elaborate but may be you would have explained to Kenyans how we are going to finance such an elaborate structure? Are we going to be paying the village councillors, are we going to pay the people who are representing people in the location, how are we going to support that?

Ya pili ni mambo ya higher education, lakini nimeaona kama kuna mahali imeguswa lakini pengine it would have been made clear. Tunasema kutoka district level, to the level of secondary schools halafu kutoka pale who is now supposed to support the higher education?

Ya mwisho ni mambo ya judicial structure, nimeona mambo ni mzuri ya Kadhis courts ni mazuri, ambayo imekuwa constitutionalized. Shida kwangu ni what about the traditional courts? Kwa sababu wakati mwingi utaenda kortini utasikia una-refer kwa kesi ambazo zilitendeka Uingereza miaka ya kitambo lakini hautasikia kesi ambayo it is referring to a situation in Kenya applying to the same situation like President. So hiyo ni shida yangu.

Shida ingine ni kama mimi ni Muislamu na nimekosea mtu ambaye si Muislamu how is our case going to be dealt with? Maswali yangu ni hayo tu.

**District Coordinator:** Asante sana tumekusikia yule wa tano? Karibu sana.

**Peter Chilo:** Kwa jina naitwa Chilo. Nilikuwa na pendekezo chapter two ilikuwa **end of side A**: tulikuwa tunapendekeza kwamba kwa sababu Katiba yetu pale mwisho inasema God bless Kenya. Tungependekeza kuna kile kifungo ambacho kinaongea the state shall treat all religions equal tungependekeza iongezwe ni zile dini ambazo zinaabudu Mungu. Kwa sababu madini mengi ambayo imetokea siku hizi ambayo ni ya kimaajabu. Chapter 4 nimejaribu kupitia katika draft lakini sikuiona na ilikua ni pendekezo ambayo niliisema wakati mwingine hapa, kwamba kuna tatizo katika Tana River yetu kwa jumla. Watoto wanamaliza mashule hawapati ID card kwa wakati na huenda ukaka zaidi ya mwaka hujapata kitambulisho, mtoto nafasi ya kazi imepatikana hana kitambulisho, itabindi akae jina lake lipotezwe. Kwa hivyo napendekeza mtoto anapozaliwa ujue kuna aina ya kibali ambacho kitamruhusu yeye kutabulikana kama mwanakenya kabla ya kufikisha miaka kumi na nane ili akaweze kungojea ile picha awe ile ingine anaweza kuitumia kufanyia zile transactions za kufuatia kazi.

Chapter 5 mahali kwa Bill of Rights, mahali kwa elimu, tulikuwa tunapendekeza, ikiwezekana pia kuwe na free education, katika secondary schools na ikiwezekana pia kila jamii iko na mtoto ambaye amekuwa na uwezo wa kuenda university ipewe nafasi kati ya watoto wawili au wanne, iwe hiyo ni free education tunalipa revenue ya tax nyingi sana.

Chapter 6 hiyo haikuwa katika draft lakini naipendekeza ikiwezekana kuwe kuna hali ya kujulikana, pia tunaita ballot papers, masanduku ya kura, katika vituo vyote ambazo zinahusika na kura kuwe na kujulikana, ili ku-avoid mambo ya rigging kuwe kunajulikana kwamba kituo cha Garsen pengine kuna makaratasi mbili elfu masanduku mia mbili, ili kufanya ile shuguri iwe transparent na hali ya kueleweka kwa watu wale wanaohusika na kura.

Chapter 6 section 97 (1) inasema tulikuwa tunapendekeza kwamba tuna-insist kwa sababu yule mwenzangu alitangulia kusema tunasihi kwamba heli tuwe na viama vitatu ili iwe rahisi kwa kufanya funding, kitu namna hiyo.

Chapter 5 Section 57 tulikuwa tunapendekeza kwamba it should specify kwamba zile treatment ambazo tuta-receive , zile emergency treatment kwa sababu mmesema mtu ako na haki ya ku-recieve emergency treatment, lakini haiku-specify ni situation gani za afya kwa sababu hapa imesema tu mtu ako na haki ya kupata matibabu ya dharura lakini katika situation gani kwa sababu kama hapa kwetu, hospitali za serikali ndizo hizi, zingine hazina dawa mtu akitaka kwenda Hola atakufia njiani (inaudible) hospitali zingine za serikali. Kwa hivyo napendekeza ziwe specified kama hapa ni private, wapi, na Serikali iweze kugharamia hiyo huduma ya dharura.

Chapter 12 Section 251 (6) nilikuwa nasema kwamba the President should not be allowed to remove the governor and this I

feel should be discussed in Parliament. Na pia kuna section 251 subsection 6 Chapter 12 Section 251 (6) inaongea kwamba President to appoint the Governor na pia atapitishwa na Bunge lakini sasa twapendekeza kwamba kwa sababu haija-specify na pia kuna vifungu vingine kama hivi ambazo zimesema the President shall appoint and Parliament shall approve. Lakini sasa pendekezo ya vifungu kama hicho kimoja, hicho kwamba President pia asiwe na uwezo wa kumtoa au kuwatoa wale anawa-appoint. Kama kuna kifungo kimoja katika kile cha Police Commissioner pale, imesema kwamba President ata-appoint na hatakuwa na uwezo wa kumuondoa ule Police Commissioner. Kwa hivyo napendekeza vile vifungo vingine viwe na vice versa ianzie Parliament ndiyo President awe amekubalika kumtoa ule Governor, wale wengine ambao anawachagua.

Na kitu cha mwisho nimesikia ukisema pengine kama nime ku-quote right ni kwamba Katiba hii pengine huenda ikatumika baada ya miaka mitano hatujui kama nimesikia Bw Commissioner akizungumza. Kama pengine itakuwa after 5 years hatujui. Lakini uchaguzi mpya tunapendekeza katiba mpya itumike katika uchaguzi mpya. Kwa sababu itakuwa ni hasara tumetumia billion nne na hatuwezi kuona manufaa mpaka baada ya miaka miaka mitano itakuwa kwetu ni hasara. Asante.

**District Coordinator:** Haya asante sana. Yule mwingine alikuwa ni nani? Hao ni wanne hao, yule wa tatu hakuzungumza, kwa hivyo ni wanne. (interjection) Yuko yule number tano? (noise in the background) Six ni nani? Haya endelea.

**Nathaniel Kiunga:** Majina naitwa Nathaniel Kiunga. Mimi nina mambo matatu tu ambayo iwapo sikuyachukua number katika hii mswaada lakini pengine nikitaja mnaweza mkajua. Kwanza ni upande wa dini. Upande wa dini, nimeona imeandikwa vizuri lakini kuna pahali pamoja niliona parekebishwe. Sijui kwamba Commissioner akienda Nairobi ataweza hapo akaangalia. Kitu chenyewe nilikuwa nataka kusema kuna waumini wa dini zingine wanaingilia vitabu vya kabila zingine wakaanza kuvitoa makosa ovyo ovyo na kuwatukana wale manabii wako katika hicho kitabu Kwa hivyo ikiwezekana pahali hapa pawekwe, kwa sababu kesho yake kutatoka vita vya kindini kama kule upande wa Sudan walivyofanya.

Kitu cha tatu ni kuhusu wilaya. Nimeona kwamba tuongeze kitu kimoja. Mambo ya kutokea vibarua katika wilaya fulani, ikiwezekana mkirudi huko muangalie mahali kuna vita kati ya wageni wa wilaya hiyo na wenyeji. Wenyeji wanaweza wakaandikwa katika kampuni fulani aje afanye kazi baada ya siku mbili anafutwa kunawekwa wengine wakutoka mbali. Kama juzi kumetokea vita hapa vilichira kwa shauri ya wageni kutoka mbali wenyeji wakaanza kufutwa makazi. Kwa hivyo hicho kifungu kiwekwe katika mamlaka ya wilaya, kata na vijiji kwamba wenyeji ndiyo wakwanza wapewe kazi pale. Kama ule ujuzi hakuna mahali hapo ndiyo mgeni wa ule ujuzi aletwe hapo. Nafikiri itakuwa ni vizuri. (clapping)

Upande mwingine in habari ya elimu ya watoto. Kweli tumeona ni watoto. Ningetoa mfano mimi mwenyewe wakati wa ukoloni ingawa tunasema wakoloni waende muafrika atawale, yaani mau mau, lakini nimeona ya kwamba elimu ya siku hizi haifai watoto wetu. Ingefaa wafanye kama vile walikuwa wakifanya. Mtoto anasoma Primary kutoka standard one mpaka std. 4 akifika std 5 mtoto yule apewe ujuzi wa kazi ya mikono kama kupiga lada, kunjenga nyumba aanze kutoka std. 5 mpaka std 8. Ili mtoto yule akitoka awe na ujuzi kuliko kuweka vyuo vya kazi sijui wapi mzazi tena agalamike pale pale primary, mzazi

awe tayari kutoa ujuzi pale kuwa na waalimu ambao wanajua hiyo kazi hii ya mikono kama vile walikuwa wakifanya. Asanteni. (clapping)

**Com. Salim:** Nafikiri ningependa kuwajibu hawa ndugu zetu watano waliouliza maswali kwanza kabla ya kuendelea mbele, mara huenda nikasahau maswala yaliyokwisha ulizwa kitambo. Mwakubali sio? Ili wale wale ambao number 6 kwa mfano sasa wale wale ndiyo watakao fuata baada ya kuwa jibu hawa. Mtaniruhusu kufanya hivyo? Sawa. Kwa hivyo Bwana Katana maswala yako ama comments zako tumeyasikia ungependelea kuwe na affirmative action, kwamba Tana River ifikiriwe imebaki nyuma miaka yote hii ungependa kuwe na maendeleo. Na unauliza hii Constitution, imo nini hapa ambapo Tana River itafaidika nayo? Kuna mengi ambayo yako hapo. Siku taja wilaya ingine hapo tumesema kwamba kuwe na Serikali ya Wilaya katika kila wilaya. Tana River District itakuwa na Serikali yake sasa tegemeo ya hio Serikali kufuatia hii sheria itakavyo fanya hiyo kazi. Yaani hapa tumeanza ukrasa mpya kabisa au tunapendekeza tuanze ukrasa mpya katika kila district, district ambayo haikufaidika au ilifaidika. Na tunasema kwamba katika kila district kuwe na serikali yake sasa tegemeo ya hiyo serikali ya Tana River District itakayofanya kazi imepewa jukumu ya kufanya kazi imeambiwa kwamba ikusanye kodi katika district hii. Ifanye mipango pia ya maendeleo – Economic Development Plans, imepewa jukumu ya kufanya mipango yake yenyewe.

Kwa upande wa pesa imeambiwa kwamba mtapata pesa zenu ambazo mtakusanya hapo. Kuna mifugo hapa kutakuwa na cess, kutakuwa na serikali inapendekeza kwamba kila mtu mwenye hili au lile atalipa kodi kiasi fulani, mtafanya mipango yenu ya kukusanya pesa.. Kisha serikali ya kati- central govt. itakuwa kama nilivyo eleza. Ni mali ya asiri ile, ya utalii mali ya utalii ya chini maji, mali ya bahari mali ya patikana ile income kutoka kodi ambayo itakusanywa Nairobi yote itakuwa ni mali ya umma. Kwa hivyo kila district pia itapata sehemu yake. Na kama nilivyosema pia, kila district itatasamwa hali yake yeye inamapato yake ya kutosha yenyewe kiasi gani. Inapopulation kiasi gani? Mapato yake ukilinganisha na mapato yako je mwananchi au raia katika eneo hilo ataweza kwa hakika kuishi au kupata maisha mazuri au la?

Kwa kufuatia uchunguzi huo au vipimo hivyo vitawekwa Tana River District itapata pia sehemu fulani kutoka treasury kuongezewa zile pesa ambazo zitakusanywa pale. Hiyo ndiyo jawabu naweza kumpa. Pia kama nimesema kutakuwa na baraza, kutakuwa na Economic and Social Council ya nchi nzima. Kazi yake itakuwa ni kubwa sana kuchungulia hali ilivyo katika Tana River District. Tumezunguka kule, tumepitia kule tukakaa siku tatu, siku nne tukaona kwamba tukawa pekishini pesa zao income yao tukaona income yao haitoshi wanahitajia pesa zaidi. Tumewapa kiasi fulani mwaka huu this financial year, nafikiri financial year ijayo afadhali iongezewe kwa ajili ya sababu moja, mbili, tatu na kadhalika. Kwa hivyo kutakuwa saa zote moderation and monitoring. Mambo itakuwa ikipelelezwa, kwa hivyo serikali ya wilaya ina jukumu na muhimu kuwa ifanye kazi uzuri, na kukiwa na matetezo yeyote, ni viongozi wa pale kuhakisha kwamba matatizo yao inafikishwa mbele na watetee mswaada kubwa zaidi. Kwa hivyo tunajaribu kusahau yaliyotoka zamani tuanze ukrasa mpya. Na kila district ukianza ukrasa mpya na pesa kugawanywa from the National cake to the District – district zenyewe kuanza kupika cake yao pia, together they should be able to make headway.

Kisha umezungumzia, mambo ya different commissions, tume bali bali tumesikia kutakuwa na tume hii tume ile, je, watu wa Tana River District tutakuwemo hapo? Hapo ni jambo la detail kwa hakika hatukusema kwamba kwa mfano Tume hii wanachama wake watatoka that district or this district it is not said. Hiyo ni matter of detail. Tumesema kwamba kabira ni ya katiba ndiyo sheria ya baba, kama ujuavyo you are a lawyer. Sasa sheria baba atakuwa na mtoto au sheria watoto ambao watafikiria all sorts of other things related to the constitution, inahusika na constitution. Kama nimesema hapo awali tukishaipitisha hii katiba, lazima pia tuchungulie sheria nyingi sana zinazohusika na ustawi na kadhalika. Sheria hizo lazima zibadilishwe pia ili zilingane na history. Kwa hivyo ile kugawanya tume hii itakuwa na wanachama wale au wale itakuwa ni kujitetea pia. Kutakuwa na wajumbe kwenye Tana River District, kutakuwa na wajumbe wenzao kutoka Lamu hapo jamani tume hii wengi watoka eneo hili, lazima Tume hili nyingine ibalance ile ingine it is a matter of figures na bila shaka huo ukija mambo itafanyika kwa uadhilifu.

Kati ya maadiri tuliotaja ni equity and justice. Kunayo tume ambayo inaitwa administration of justice, Human Rights and Administration of Justice. Mtu anaweza akashtaki hiyo akasema hapa hakuna administration of justice. Tana River ukilinganisha na district nyingine utaona kwamba imeachwa nyuma. Hatuna watu wa kutosha katika tume zote zile, ukitazama wengi kutoka hapa au kutoka pale. Kwa hivyo muhimu ni mtu kujitetee, district kujitetea na wajumbe wake, wabunge wake n.k. members of the council, govt. council to claim those rights and to fight for them. That’s all what I can tell you. Lakini hatuna details hapa ya kusema tume hiyo wanachama wake ni kumi na mbili hao wanatoka huku lazima watoke kule au kule, we have not done that. It is a matter of details

Pia public expenditure is a matter of detail. Inategemea ile budget of that year na ukumbuke kwamba budget itapitishwa kwenye parliament na hapo ni mambo kujitetea na fulani kundai mtu ajue kwamba Tana River District itafaa kiasi fulani na kwa nini kiasi huku district zingine imepewa zaidi. What is the rational for that sort of a thing.

Foreign aid and public debt tumekubali kwamba jambo hili ni muhimu sana ukitazama page 30 tumezungumzia si public debt yenyewe lakini tumesema kwamba serikali ikitaka kupata mikopo lazima ifuate masharti fulani. An Act of Parliament, kuwe na sheria ya bunge ambayo itaonyesha the terms and the conditions of the laws na terms hizo, masharti hayo ya mkopo lazima yawekwe mbele ya bunge, wabunge wajadiliane juu ya masharti hayo. Na kama hayo huliosema kwamba masharti hayo ni wazi ya julikana masharti ambayo serikali itaweza kubebe masharti hayo na mzigo, so everything is going to be open for debate. And they shall not come into force unless they have been approved by the resolution of parliament. Zamani mambo hayo ilikuwa inafanyika huko treasury, sio? Sasa lazima bunge iseme tumepata million thelathini in the world bank, masharti ya kupata elfu thelathini ni ipi? Ikiwa bunge haikukubaliana na masharti hayo yatatupwa bali and the law will be rejected ikiwa masharti ni kali sana. So that is the way it is going to be. Now it is going to be transparent and it will be the people’s representatives, wawakilishe wananchi ambao watakubali masharti ya mikopo yote maanake ndiyo hao wata beba pia gharama ya mikopo kama hiyo.

Bw. Hussein Kiribaye umetaja kwamba Chapter 4 habari ya uraia – ashaa ondoka? Nafikiri ametosheka na ile jawabu yangu nimempa kwamba ni mwananchi yule ambaye wakati wa katiba hii itakapokuwa na implementation ndiye ambaye itaendelea kuwa mwananchi. Sikusema mtu wa nje au mgeni ambaye atakuwako hapa nchini wakati wa hii katiba kutiwa kuwa sheria, si mgeni huwa automatically citizen, ni raia. Maanake kuna raia wakati katiba hii itakapokuja na kuwa sheria ndiye atakaye endelea kuwa raia this is just the legal technicality, kumlinda yule raia wa sasa. Tusianze kusema yule atakaye zaliwa katiba hii ikishawekwa ndiye atakuwa raia. Je yule ambaye azaliwa mbele ya hii katiba kuja, si raia? But for legalistic purposes, na bila shaka ufahamu the legal aspect that we have all those documentation that those who are citizens when the new constitution comes into place remains a citizen, wanabaki kuwa ni raia.

Pia ameuliza party funds, au pesa zinazopewa chama cha kisiasa, hizo zinatumika kwa njia maalum zikitumika kama nilivyoeleza hapo awali nilipoanza kueleza kwamba matumizi hayo itakuwa ni kumsaidia ile chama kupata publicity tusema kama radio au katika television au kueneza elimu ya raia, civic education. Pesa hizo hazitakuwa nyingi sana zitatumika kwa njia hizi tu, mbili na zikitumika kwa njia ambazo si hizi basi ile party lazima itatiwa adabu.

President and party. Kuna shida gani kwamba president akishatoka party na akifanywa president hatapendelea ile party. Itategemea, akipendelea atakuwa amevunja katiba, sio? Lakini kukiwa na utabiti kwamba amevunja katiba tulieleza, akivunja sheria kutakuwa na uchunguzi ikidhibitika anaondolewa. Kwa hivyo kuna protection pale.

Bw. Mureithi umesema devolution of power, je village elders watalipwa au la. Ile jawabu ni watalipwa maana wakiwa na kazi ya umma lazima wapewe malipo. Kiasi gani hatujui. Wanjua plan ya katiba sio ya kesho, kesho kutwa au mwaka ujao au miaka kumi kutoka sasa. Tunaandika katiba ambayo itandumu kwa hivyo tukisema atapaka kila mmoja elfu tatu au elfu thelathini will the same figure be of the same value in one hundered years from now? So those figures you don’t put them just for the priniciple that you will be paid for services to wananchi like everybody else who represents wananchi.

Post secondary education, nani ambaye atachugulikia? Hiyo itakuwa ni national govt. na labda mpango huu tulionao sasa wa vyuo vikuu utaendelea, vyuo vikuu vitaendelea kunjengwa na tumependekeza kwamba zinjengwe katika kila eneo la nchi na kwa hivyo hiyo hatakuwa ni jukumu la serikali ya wilaya bali jukumu serikali ya kati.

Traditional courts, tribunal, zitakuweko and that will be infact if you look at our draft constitution utaona tumetaja pia; Kadhi’s court, Magistrates courts na tribunals, ambazo zitachugulikia mambo ya kitamaduni ya kienyeji. Sawa? Pia tunazungumzia Muslims and non-Muslim courts tukiwa na kesi kati ya Muislamu na asiye kuwa Muislamu, kesi kama hiyo itachugulikiwa na ordinary court. Ni mambo ambayo ni ya Waislamu peke yao ambayo itachugulikiwa na Kadhi’s court, sawa? Tuseme hata mambo mengine tumependekeza kwamba ikiwa Waislamu wawili wanagombana kuhusu mahusiano ya kibiashara kati yao, hao ikiwa wote ni Waislamu waweze pia kuenda kwa Kadhi na matatizo kati yao yaweze kusuruhishwa juu ya sheria ya Kiislamu. Lakini akiingia asiye Muislamu hapo basi huwa si mambo ya kumhusu Kadhi ni mambo ya kuhusu secular courts, sawa?

Bwana Chilu umezungumzia state kwamba God bless Kenya hiyo ni ishara kwamba ingawa there is no state religion, Kenya is going to be a secular state lakini hata hivyo hata kati ya sisi wanatume tumesema sisi we are God fearing people lazima jina la Mwenyezi Mungu litanjwe hapo – God Bless Kenya. Tumeambiwa kwa mfano kuna wale ambao wanaabundu mashetani je hao wapewe uhuru wa dini? Hapo hatukutaja – devil worshippers, maana hatuna na legal defination of what is a devil worshipper, nani anaye muabundu shetani? Hatujui. Lakini ikiwa dini yoyote itaendeshwa kwa njia ambayo italeta mafarakano kati ya watu, na watu kupigana, basi action will be taken against any party that supports the religious body that is causing problems in the country. Maana tunajua kwamba wengine wanataja dini zingine kwamba hawa wanaabundu mashetani. Sisemi hapa nchini lakini kwingine na wanatukana viongozi wa dini zingine kusema kua hawa hawana dini hawa wanaabundu shetani. Ukifikiria nani anaye abundu shetani ni nani? Ni yule mwenye dini ambaye ni religious, yule ambaye anaingia kwenye bar anamwambia mwenzake huyu anamwabundu shetani apata kulewa, anakwenda kufuatana na wanawake wa usiku, huyu anafuata shetani. Is that so? Is he also a devil worshipper? Wengine atakwambia I am not a devil worshipper, I worship God but I have other weaknesses, so it is a very difficult term to define. And so far we haven't heard any evidence brought to us to say they are acting as devil worshippers and where are these people worshipping the devil. Like we say it is a law that can be amended in the right of experience and in the right of developments.

Tatizo la kutokuwa na kazi, tatizo la kutopata ID tumesema sana mambo kama haya. Lakini ukisoma hapo kwenye draft constitution, tunasema kwamba immediately you are declared a citizen, ukijulikana wewe ni raia, umezaliwa hapa you have a right to an ID and a passport. It is no longer a privilege to own a passport it is a right and we declare it as a right in the draft constitution.

Free education ukipendelea hiyo in Secondary schools tumeshataja haki ya mtu kusomeshwa kutoka pre-primary, primary na secondary, ni haki hiyo. So it is a question of implementing the draft. Lakini tumesema kwamba zile Basic Rights or Bill of Rights kwamba hatuwezi kuseme serikali lazima itimize kila right pale na kumpa kila mtu maskani au nyumba na kadhalika. Katika muda wa miaka miwili au mitatu kama tumefanya katika eneneo la ardhi ambayo tumeipa serikali miaka miwili, hapa hatuwezi na kuna gharama kubwa zinazohusika na kumpa kila mwananchi hizo haki zake ambazo tumetaja hapo, makao elimu na kadharika. Lakini tumesema kwamba Rais ni lazima atoe ripoti kila mwaka tumefikia wapi katika kutimiza na kumpa kila raia haki zake. Je tumepata elimu ya secondary school au bado na kadhalika. So it is a question of progressive evolutionary development towards realising these rights for wananchi. Elections na transparency of election. Tumetaja hapa kuwa elections iwe transparent. Kwamba ungetaka tu publish polling stations ziwe wapi pia itakuwa ni kazi ya electoral commission. It is in detail procedure for holding elections throughout as they normally do in newspapers, wana-publish list ya vituo vyote vya kupigia kura. So it is done already, it has been done for a long time.

Tupunguze idadi ya political parties. It is a proposal, lakini ukisoma jinsi ambavyo masharti ya kuandikisha political parties utaona kwamba haitakuwa rahisi kwa mtu kuanzisha political parties. Lazima iwe ina national outlook na party kuwa ina

national outlook sio rahisi. Iwe na members katika kila eneo la Kenya. Hiyo si rahisi, itakuwa rahisi kupata political party from one wilaya labda; Mombasa jamaa apate party pale aanzishe chama chake na kadhalika. Health treatment should specify emergency. It is a matter that can be debated lakini hivi sasa emergency treatment is provided. Muhimu ni kwamba mtu anapelekwa haraka kwenye kituo cha matibabu au katika hospitali lakini, ungependa kwenye jina liwe ni specified sio? Hilo ni pendekezo na bila shaka ni aina ya pendekezo ambalo… you have a representative from this district? When he attends the National Conference you can give him that suggestion. You can sell in your idea and I think it is sold to him kwamba kuwe na emergency treatment free in any hospital or all govt. hospitals it is something to be considered. Tukumbuke kwamba hapa tuna mapendekezo sisi ni binadamu kama nilivyo sema mwenyekiti wetu we are all human beings we have no monopoly of wisdom hatuna busara kushida mtu yeyote, na sababu ya kuja hapa ni kueleza wananchi na watupe maoni yao.

Pia tulitaja kwamba President sikuwa ana mchagua waziri tu lakini asiwe na haki ya kumuondoa pia bila approval. Nafikiri hiyo in implied, he cannot just remove a Minister as a member of cabinet. Behind the cabinet there is the Prime Minister. So the President cannot go behind the Prime Minister akamwambia amuondoe huyu. But it is something that can be looked into. (interjection: question)

**Speaker**: …. (inaudible) Police Commissioner, President ana mu-appoint, Bunge ina-approve, sasa tunasema President hawezi kumuondoa (inaudible)

**Com. Salim:** Yote tu-apply jambo hilo kwa waziri (interjection: question inaudible) Governor nani, wa Central Bank? Ok. Asante. Unasema kwamba ulifahamu kutokana na maelezo yangu kwamba the new constitution will not apply to the elections nafikiri hukunifahamu hapo. Nimesema kwamba ile sharti ya umri wa mgombeaji uchaguzi wa kiti cha rais kati ya Chapter 35 na 70 just that the age does not apply to the next election ili kwamba mtu ambaye umri wake ni sabini na moja aweza kuingia katika elections zijazo. Sehemu hiyo tu ya age does not apply for the next elections. Hii ni kuhakisha kwamba the transition period tumruhusu yeyote ambaye anataka kuwa rais. You are 71, 72 ikiwa watu wanakutaka uende. Lakini elections zitakazofuata itabidi kutumia sharti hiyo ya age. That is what I meant. I did not mean for the whole katiba will not apply to the next elections only that particular point of the age of the presidential candidate. Kuwa he must be between age of 35 and 70 that is the only thing I meant does not apply to the next election. Nafikiri ni wazi sasa. Kuna swali hapo? Hebu ngoja ni malize.

Nathaniel Kihunga - tumesema kwamba hakuna dini ya mtu ambayo itaingilia dini ya mtu mwingine na yule ambaye anasema mambo ambayo huenda ikaleta mafarakano na watu kuteta au kupigana azuiwe asifanye kazi hiyo. Kwa hivyo kutukanana kwa njia ya kidini wa kutukana dini yeyote katika hadhara ya watu au mbele ya watu itakuwa ni jambo ambalo halitaruhusiwa chini ya katiba mpya.

Pia tumependekeza kwamba kazi ikipatikana tuseme katika wilaya ya Tana River nafasi za kwanza zinapewa wenyeji wa kule hiyo ni matter of detail na kwa hivyo ile serikali ya wilaya pia ni jambo ambalo litazungumzia na wale wanaohusika kuhakikisha

kwamba, maanake pendekezo hili kwa ajili tumelipata kutoka sehemu nyingi sana na ni jambo ambalo la weza kutazamwa zaidi na mtu kupendekeza kuweko trend kama hiyo.

Pia elimu kwa hakika hii katiba ni katiba baba, ni kanuni baba au sheria baba. Chini ya katiba hii kuna kila aina ya sheria zingine kuhusu kila aina ya sehemu ya maisha yetu. Kwa hivyo kutakuwa na Education Act. Hivi sasa kuna Education Act. Kwa hivyo katika kanuni ya elimu mambo kama haya haikufanywa, tukirekebisha syllabus za school tunaweza kusema school ziruhusiwe au tuseme district ya Tana River peke yake tumeseme hivyo katika shule zetu sisi tungependa kuwe na secondary education mkapata syllabus yenu wenyewe na labda huenda ikafuatwa na wengine. Au labda mkaona kwamba za district zingine zinaweza zikafanya. Kwa hivyo mtapata ile serikali ya kiwilaya ambayo itakuwa huru katika mambo mengi sana hata katika kurekebisha syllabuses za elimu na kadhalika.

Nafikiri hao ndiyo watano wa kwanza. Sasa kwa haraka kabisa tafadhalini wale jamaa ambao wamebakia watano au ni wanne? Hebu tafadhali mkainue mikono (starts to count) watano. Kwa hakika hatuwezi kuendelea sana saa zetu zimekwisha. Tunasafari ya kurudi na nitachukua wale wanne waliobakia katika hesabu ya kwanza. Ni wanne au watano? Unawanjua? Huyu ni watano, huyu ni wa saba sasa kisha wa nane wa tisa na wa kumi? Haya.

Speaker in the background ( inaudible)

**Yahaya Swabir:** Jina langu naitwa Yahya Swabir, Councillor kutoka Kipini. Maana yangu ijapokuwa pengine nilichelewa kidogo kuingia labda kuna baadhi ya mengi yalionipita ambayo hayo yalizungumzwa sikuyafahamu. Kitu cha kwanza ningekuwa na ombi langu kwamba Minister, Bw. Com. alisema Minister sasa sikuelewa kuchaguliwa Minister atakuwa kwa Bunge ama atakuwa nje ya Bunge?

Basi kama atakuwa nje ya Bunge, maoni yangu ni kwamba Minister awe Mbunge ndiyo aweze kuchaguliwa Minister. Kwa sababu, Minister akiwa nje ya Bunge, kitu cha kwanza atakuwa yule mtu hajafai kuchaguliwa kuona uchungu ambapo ile ministry inatakikana ifuatiliwe kikamilifu. Lakini Minister akiwa Mbunge ako na uchungu kwa sababu yeye amepigania ubunge, ameona ile shida ya Bunge basi akiwa Minister atakuwa Minister mzuri. Oni langu la kwanza.

Oni la pili Bw. Commissioner umesema kutakuwa na majimbo ya district. Ningependelea pia kuwe na majimbo ya province kama ma PS. Utakuta kuna ma-PS ambalo kwa province ni moja imetoka ma PS kumi na ukiangalia kama mkoa wa Pwani utakuta hakuna PS au ni mmoja peke yake. Pia usawa wa ma PS katika majimbo hilo ni jambo liangaliwe.

Kitu cha pili ni Kadhi, umetuelezea Kadhi, Chief Kadhi anataka experience ya miaka kumi ndiyo awe Chief Kadhi. Na umesema Kadhi awe Kadhi anatakikana experience ya miaka tano, sasa hiyo experience atatoa wapi ikiwa hakuwa Kadhi? Na kitu kingine ni kwamba kama Chief Justice, anapewa gari anapewa ulinzi anapewa…. Mambo mengi anapewa na serikali.

Sasa utakuta Chief Kadhi gari hata baiskeli hana anatembea na mguu ambapo yule ni Chief Justice na huyu ni Chief Kadhi, kuna tofauti ya kusema, lakini wote kila mtu amesimamia ma-judge wake au mahakimu wake. Kwa hivyo kuwe na usawa hapo.

Halafu pia kutakuwa na Rais, halafu kutakuwa na Prime Minister, ni maoni yangu kama Rais ametoka kwenye tuseme dini Fulani Prime Minister atoke kwenye dini nyingine. Kwa mfano kama Tanzania utaona kama Rais akitoka bala makamu wake anatoka kisiwani. Kwa hivyo kama Rais amekuwa Mkristo Prime Minister awe Muislamu. Kama Rais amekuwa Muislamu, Prime Minister awe Mkristo hilo ni katika ombi langu. Na vile vile, nyumba moja kama kumekuwa Rais, kwa mfano kama nyumbani kwetu mimi nimekuwa Rais wa nchi basi katika nyumba hiyo, mtoto wangu mpaka mjukuu wangu kulingana vile tutakwenda hakuna Rais anatoka kwa nyumba hiyo tena. Kwa sababu kama nyumba hiyo hiyo kutatoka Rais, Rais lazima atakuwa Rais siku zote atakuwa kwa sababu watakuwa matajiri, wako na pesa na ile nyumba ambayo haina pesa haiwezi kuwa kwa sababu nyumba hiyo haina pesa. Na mambo yetu ya Kenya tuna mambo mengi … kwa hivyo nyumba moja ikitoka Rais hasitoke tena Rais mpaka mwisho wa ulimwengu huu. Asante sana Bwana Commissioner. (clapping)

**District Coordinator**: Mwingine atakuwa huyu mzee hapa.

**Kayo Ahamed**: *Bismillahi Rahmani Rahim*. Jina langu ni Kayo Ahmed. Sasa nafikiri kila mtu anasema amepata uhuru. Sasa kama mtu hapana jua lugha ya taifa nafikiri ana uhuru wa kutumia lugha ingine nafikiri yeye anaweza kutafuta mtu wa kutafsiri hii. Kwa katiba kila mtu apate uhuru na katiba inataka kila mtu hawezi kujua lugha ingine anaweza kutafsiriwa, kuongea lugha ya Somali au lugha ya pahali pengine (speaks in Vernacular) *Waxa chirta mey layirathi Gumbo oo location mithca kamith iney iyagu wakil ee igadigten dhathki fadien*

**Translator**: Mzee anasema yeye amechaguliwa na wananchi wakutoka mahali ambaye inaitwa Ngumu ambaye ni sehemu ya Muira location ili alete maoni yao.

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhathka iyaka ee wexey aath iyo aath ee sheg ugakavan yacni uhurutha ee katibathan wadhanka kadacthey ama Kenya xatha lasubinaye iney waxva ee kulexein oo weli iyaka kaxelen oo yar rasimal caa oo cakal ee oo weli ee kaxelin*

**Translator**: Wananchi hao wanalalamika sana kuhusu ile katiba End of tape 2

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhathka iyaka ee wexey aath iyo aath ugu dib kavan waxa oritha xaga dhowlatha oo masomo layiratha ee kaxestan malex laakin xaga dhinta islamka iyako xoga uu kava oo masomo kabaxasaneya oo Qur'anka islamka oo macalimin culuma cee ama Sheikh uu xaisto oo madarasa kasubsathey laakin waxa ee kavan malex dhathka oo dhowlatha xagethe oo waxa masomo ee kuxestan malex dhathkas sii aath iyo caath ayei dib ugu kavan.*

**Translator**: Anasema kwa upande wao, kwa upande wa masomo wana shida sana, sana sana upande huu wa shule wako na shida lakini upande wa kidini wanatia bidii yao na wanapata kusomesha watoto wao

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhathka iyaka ee wexey masomo ugu ceysanin dhowlatha markey mesha layiratha Danis layiratha sagashan iyo sagalka ee karartey oo mesha ee geyse waxtiga inta wexey uu waregeyen cilmoxothi iney caxris xelan oo masomo xelan marka ila locationka oo jeneka oo dhowlatha uu xilsaratey ila ninka oo uu joga ila divionska oo dioga ka xilsaran ila DC ga melkasta dacwa chirta iney yacni skul ee cexelan cilmaxa ee caxris ee xelan. Amrka intas wei surta geli weyse iney skul caxrisathan wey wayen, marka wexey kavan xormarka Kenya ee gareyso si ath iyo ath ayei ugu thambeyan.*

**Translator**: Anasema wamepeleka malalamishi kwa kila ofisi, division walipeleka, kwa district kwa idara ya elimu ili watoto wao wapate kusoma lakini mpaka saa hii hakuna mafanikio yoyote wamepata.

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhatka iyaka ee wexey aath iyo ath ugu musten ila afar boqol cunuk iney masomo ee taxai.*

**Translator**: Watu wao katika kile kijiji idadi ya watoto inaweza kufikia mia nne na hakuna hata mmoja anasoma

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhathka iyaka ee waxa ee yixin ee bathi usubsathen iney afar gilas oo iyaka gacantoth kusubsathen oo nursery ee ee kadisten mesha oo iyaka xolaxa laacta labaxayen ila boqol iyo sithetan cunug.*

**Translator**: Watu hao wamejitahidi wakajenga darasa nne wakawa wanapeleka watoto wao kule wanasomesha watoto wao wakitumia pesa yao binafsi. Watoto mia moja themanini.

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhathka boqol iyo sithetan cunug markey caa markety ninki dhowlatha wakil uu caa mesha udigi wuxu yiri wax meshan caxath kalexethen malexe dhath oo wachachira oo markey mesha fadistan wax ee lamareysin oo cilmaxa wax caxriseyna malex.*

**Translator**: Sasa yule mtu, yule kiongozi wa Serikali aliokuwa pale aliwaambia wao ni wageni kwa hivyo wasiendelee na masomo yeyote pale, wakae tu kama wageni pale.

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Dhathka iyaka ee sii aath iyo aath wexey uguthambeya xaga oo caxriska ee marka waxan kacothsaneyna katibatha markey ee taxai kabilaxa yar yar oo koriska oo wadhamaxa oo yacni oo yar oo kavilaxa we wei exen iney yacni waa xagotha ee kaxelan wadhanka Kenya.*

**Translator**: Anasema hao watu wako katika wale makabila machache sasa kwenye hii katiba mpya anaomba iwe inawapatia haki ya kutosha vilivyo yaani hao makabila wachache ambao sio wengi wawe wanapata haki yao vilivyo.

**Kayo Ahamed**: (vernacular) *Sasa waxan kacothsaneya dhathka meshan fadiya xata ila xayatha wei cathen caxris yacni skul si ee cuxelan mesha dismo cee waxan othsaneya katibatha dhathkas iyaka si aath iyo aath uu weliva mesha layiratho waa iney katibatha ee uwato kabilka isaga oo kavil layiratha gel checel oo ath iyo aath mesha ugu taclotho caxris xagis.*

**District Coordinator:** Kuna akina mama hapa njoo tafadhali. Ni wawili, kuna huyu Sera na yule mwenzake ako wapi? Yule alikuwa anataka kuzungumza ni wewe?

**Esther Dulu:** Asanteni sana. Mimi kwa jina naitwa Esther Dulu, Chairlady wa Maendeleo ya Wanawake Kipini Division. Maoni moja ambayo tulikuwa nayo Kipini ni kuhusu wadhifa wa President, kwamba Kenya si kabila mbili, mara ya kwanza ni Mkikuyu, mara ya pili ni Mkalenjin na hata saa hii tumechanganyikiwa. Kwa hivyo kulikuwa na maoni kipini kwamba mara hii kukiwa kabila hili mara nyingine kabila nyingine nalo lipewe nafasi. Kwa sababu hiyo tungeonelea kwamba yule President angetakikana kupigania wakati huo achaguliwe na Wabunge wenyewe. Sio mtu mmoja aweze kumchagua kado ya vile anavyotaka. Na kwa sababu hiyo kama kabila ndogo pia, zitapewa nafasi kutakuwa na mashindano kama kabila jirani amepata President kwa sababu ya huduma zake zimependeza kwa wananchi na serikali kwa hivyo na sisi hebu tufanye bidii ili na sisi tuwe tutachaguliwa siku nyingine tutumikie huo wadhifa. Lakini tukitegemea kabila moja tutakuwa wanyonge na wengine hatutapata nafasi na kura tunapiga sote.

Vile vile tulikuwa tumetoa maoni kwamba viongozi wote ambao watatuongoza katika sehemu tofauti tofauti yakiwa maongozi yao ni ya kutuzaidia basi kiongozi kama huyo tumpitishe kwamba hatatufaa. Kwa sababu anatuumiza sisi bado tunamshika tu, anatuumiza tunamshika tu kwa hivyo tumeonelea kule Kipini kuwe na vote of no confidence kwa kiongozi yeyote ambaye hatatekeleza shuguli na hali za wananchi.

Pia tunajua kwamba tunaleta pesa za aina tofauti tofauti. Saa hii pesa nyingi zinapelekwa ofisi ya district na zingine katika sehemu tofauti tofauti za division na constituency hatuzioni. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba, kama kutakuwa na pesa ya kuletwa katika eneo la maendeleo ya wanawake, vipofu, wasiojiweza tungetaka hawa wanavikao ama wana account zao kwa division ama constituency, wakipitisha kwamba pesa hizi ni cha huduma ya maendeleo ya wanawake basi lile fungu la division ama constituency liweke katika ile account ya constituency na viongozi wa serikali, na wale akina mama watakaa pamoja kuangalia ni vikundi gani vilivyo katika constituency yetu ili wagawanyiwe kwa hali ya usalama. Kuliko hali zote zinaenda kwa district level. Hata saa hii tunajua kuna pesa inaitwa eradication of poverty ambazo zimekuja na mpaka saa hii wengi sana tunasisikia ni habari na ndoto, lakini hatujaziona katika vikundi, division, ni habari. Kwa hivyo hata saa hii tunaunyonge, wamesema wameleta hizo pesa kupunguza umaskini lakini bado umaskini unaendelea sababu pesa zimeshikwa, na ukizitaka unaambiwa nipe proposal, application, na zinafanywa na hatuzioni. Sasa ninaona pesa ziko bado, lakini naona kwamba viongozi hao wakati mwingine kuzitoa akijua kwamba kikundi hiki ama constituency hii huyu anayeshugulika ni ndugu yangu, mtoto wa mjomba, shangazi wanapata. Lakini wale wengine hawana mtu pale wao unasikia uandike application, andika proposal. Kwa hivyo ingekuwa vizuri zigawanywe kwa division ama constituency na wakuu hao washugulike na wale viongozi wa akina mama ama ile section ili wapate kupata hivyo.

Kuna funds saa zingine zinatoka za national kama zile tutaenda kwa kura saa hii. Wakati tunapoanza kazi hizi tunaambiwa kwa

mdomo makarani ni shillingi kumi, presiding officer sijui ni nini. Kisha basi kile kidogo wanachotuambia uwa hawatupi kwa amani huwa ni matatizo, nikuenda kufuatana, unaenda kortini na pesa hazitoki. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba kazi kama hizo zinapotokea zitangazwe kwa maradio kila mtu ajue nitaandikwa karani, pesa zangu ni shillingi mbili, kwa mwezi ni shilling inne, kwa mwezi fulani. Ninasema tu hivyo kwa sababu hiyo kazi nimefanya mara mbili na tulikuwa na mararamishi mpaka zingine zikapotea. Na pia kama ingewezekana basi wakishafanya hizo kazi walipwe, siku ile ile ya kwanza ama ya pili kisha itakuwa wewe unafanya ile kazi mbila wakimaliza hakuna malipo tena wala hakuna kupumua

ID tumesema kama kadi za kura zitaendelea kila siku, na ID ziendelee kwa sababu watoto wetu saa hii wanakosa kuandikwa kazi, kwa sababu hawana ID. Na imekuwa vigumu F4's wakati huo anang'ang'ania kazi hapo kazi zenyewe zimetoka lakini unaulizwa ID, huna. Kwa hivyo sijaelewa ni kwa nini hata kama wale watoto wa Form 4 wa kila mwaka wanatoka form 4 term 2 wahakikishiwe ID wamezipata, term 3 ikija kila mtu ako na ID yake anaweza kujisaidia na kufanya kazi. Sio term three watoto wanatoka kuenda maporini ndiyo anaenda kuitafuta.Unapata mahali huna ID kwa hivyo form 4 waangaliwe term 3 wapate ID zao Na … (interjection: la mwisho?)

Campus intake, saa hii kabila ndogo ndogo wanadhurumiwa kuchukuliwa katika elimu ya campus, university. Mtoto anaingia mtihani anapata 'A' combination za sciences lakini kwa sababu ametoka kabila ndogo anachukuliwa na art combination. Saa wakati ukifika mtoto analilia kitu chochote cha bunge ama cha ofisi kubwa akiangalia kibali chake ni art na art katika wakati huu haina market na hata akichukuliwa labda ubunge kwa sababu elimu yake imeingilia kwa Art inakuwa vigumu mtoto kama huyo kuwa considered na hana elimu ya kutosha. Kwa hivyo kama mmeamua kusaidia kabila ndogo ndogo mtusaidie kikamilifu. Na mmeyapanga yote lakini hamjatuambia kwamba wale watakaokwenda kinyume cha sheria zinazo pangwa ni hatua gani watachukuliwa? Kama ni mtu amefanya ufisadi akaiba million ishirini na amewachwa hivyo hivyo ama pengine aambiwe sasa wewe huna kazi. Ni hatua gani serikali itachukuwa kwa wafisadi wote wale tunaumia, tunaumia ya kutosha. Asante.

**District Coordinator:** Nafikiri tumefika mwisho kwa hivyo tumsikize Commissioner atupatie jawabu wakati umeenda sana na hata yeye anataka kusafiri kwa hivyo tafadhalini mtuie radhi.

**Com. Salim:** Samahani kwa kuwa hatuna wakati wa kumsikiza kila mtu mwenye swala tungependelea sana kukaa kuendelea lakini tuna safari yetu ingine ambayo lazima tuifanye na kujitayarisha kwa safari hapo kesho kwa hivyo mpango wetu hauturuhusu kukaa zaidi. Lakini ningependa sana kila mmoja ambaye ana swala atupe swala la kuandikwa. Yule yeyote ako na swali anaweza kutuandikia na wakati wa kuandika akatupa swala lake au pendekezo lake la kubadirisha jambo lolote katika mswaada huu wa katiba. Tutayari kabisa kupokea mapendekezo hayo au swala hilo kisha tukawajibu kwa njia ya posta. Hiyo tunaweza tukafanya. Kwa hivyo wakati nilionayo sasa nitatumia kujibu hawa wandugu wameuliza maswala.

Kwanza Bw.Yahya Swabir ungependelea kwamba Minister awe ni MP. Pendekezo ni fikira na mawazo kila moja ana pendekezo lake. Sisi kwa sababu ya kumuweka waziri mtu wa nje tunasema kwamba awe yule MP anashugulikia wale

walipeleka yeye kule Bunge. Kwa hivi sasa MP akishapata idara au kuwa na jukumu yakushikilia wizara huwa hana wakati wa kushugulikia na kutumikia wale ambao walimchagua hapo awali. Kwa hivyo tungependelea waziri awe kutoka nje.

Pili upande wa Provincial Govt. tunasema hakuna – hatukutaja hapa Provincial Govt. kuwe na Provincial Govt. Kwa hakika ukisoma vizuri kutakuwa na Provincial Council bali na District Council. Kila District itapeleka wajumbe wa wakilishi kwenye Provincial Council. Kutakuwa na Provincial Administrator, na kazi ya Provincial Council headed by Provincial Administrator ni kwamba baraza hilo la jimbo litashugulikia kazi ya kupepeleza mambo kwenye district na kufanya mipango kusaidia kila district iliyoko katika hiyo province. Kazi yake itakuwa ni coordination, pia kufanya mikutano kutokana na waakilishi wa kila district provincial council itakuwa ikizungumzia mipango ya maendeleo katika province nzima. Kwa hivyo kuna nafasi pia na kuna mamlaka pia imepewa provincial .. lakini si mamlaka kama ile ya district council hii ni liason, coorporation, kwa mfano provincial council itahimiza au kuhamasisha district mbili, tatu kushilikiana katika maendeleo. Tana River ishirikiane na Lamu District wakikutana pamoja wanaweza fanya mikutano yao pia. Lamu District na Tana River District wakutane Hola au wakutane Lamu town kuzungumza juu ya barabara ambayo iko kati ya district mbili ili istawishwe kwa njia iliyo bora zaidi. Kwa hivyo kuna role hapa ama kazi ambayo inaweza kufanyika na Provincial Council pia. Nafikiri mumenifahamu.

Na tatu unasema kwamba Chief Kadhi ten years experience ikiwa hatachaguliwa experience hiyo atapata wapi? Tunasema ten years experience as an advocate of the Hight Court. Awe ni wakili ambaye ameshugulikia kazi za wakili au mwanasheria kwa muda wa miaka kumi. Kwa hivyo Chief Kadhi atachaguliwa kati ya wale wanasheria waliojihusu sana au walio jishikilia kwa njia maalum elimu ya sheria na wako hapa hapa nchini. Moja kati ya wanatume wetu ni mwanasheria ambaye amejihushisha na elimu ya sheria na mtu ambaye ana experience. Si semi kwamba huyu atafanywa Chief Kadhi kesho, la. Lakini nasema kwamba wako. Wanasheria wa Kiislamu ambao wamesomea sheria ya Kiislamu na wamekuwa mawakili wa muda kutosha kuwa Ma-kadhi na Chief Kadhi.

Pia pendekezo lako ni kwamba ikiwa Rais ni Muislamu Prime Minister awe ni Mkristo vice versa. Mapendekezo kama haya pia tumepewa kama ikiwa Rais ni mwanamume Vice President awe ni mwanamke Lakini tungependelea kwamba elections zifanywe kwa yeyote ataka kujaribu ajaribu. You never know there will be another Ngilu tomorrow who will become the president au Muislamu Kesho akatokea akapata kura za kutosha asiye kuwa Muislamu akawa President na kadhalika. Au Mkristo ambaye anapendelewa na idadi kubwa zaidi na Waislamu awe ni Rais kwa hivyo tunasema nchi yetu itakuwa ni secular state nchi ambayo haina dini maalum. Dini zote ni sawa Kwa hivyo lazima cheo kama hiki kiwe ni cha Kenya yote, Muislamu, Mkristo, Mhindu na kadhalika.

Bw. Kayo Hamed umezunguza kwa urefu, ameondoka? Tumeyasikiza malalamiko yake na nataka niseme kwamba eneo ambaye yeye anakalia na watu wake wako katika District maalum sio? Kwa hivyo itabidi ile District ikiwa Katiba hii itakubaliwa itakuwa ni jukumu la District Council or District Government ya Tana River kuhakisha kwamba yeyote aliyoko katika eneo lile anapata elimu. Kama nilivyoeleza, mamlaka au jukumu kati ya mamlaka yake itakuwa ni kueneza kusimamia

elimu katika eneo lile.

Bi. Ester Dulu umeuliza President awe kutoka kabila hii au ile sio kila mara President anatoka sehemu moja, sasa inategemea wananchi wenyewe vile watakavyo hukumia mambo hatuwezi kusema President akitoka kabila moja asitokee tena katika kabila lile kwa muda wa miaka tano au kumi ishirini n.k. Hiyo itakuwa kumnyima mtu yule haki yake ya kusimama. Yeyote ana haki ya kusimama kuwa Rais. Kisha itategemea wananchi wenyewe vile watakavyo hukumu sio? Ikiwa raia walisema huyo tulipata mmoja kutoka kabila hiyo hivi karibuni hatuna haja ya rais kutoka kabila ile kisha wananchi watapiga kura kumpigania mtu mwingine wakitaka au kumpigania mtu kutoka kabira lile lile wakitaka pia. Kwa hivyo hatuwezi kumuingilia mwananchi katika … ama kusimama kama Rais ama kuchaguliwa na wananchi. Wote wako na confidence katika kiongozi wowote, sio? Basi vote of no confidence lawezekana. Tumeeleza jinsi ambavyo Rais anaweza kuondolewa, kuna njia ya kumuondoa ikiwa amevunja sheria kubwa yaani katiba itaondolewa ikiwa anafanya kitendo kibaya sana, pia atafanyiwa uchunguzi iki idhibitika ataondolewa.

Mbunge pia anaweza kuondolewa ikwa watu wenyewe katika eneo fulani wamesema kwamba huyu ni mbunge wetu hafanyi kazi na ikiwa theluthi moja, 1/3 ya wale wapiganji kura katika eneo lake wataandika petition, 1/3 ikiwa eneo lake kuna watu elfu tatu, elfu moja wakaandika petition kumpelekea speaker huyu hatumtaki tena sisi amefanya hivi na vile na vile ametusahau mpaka wa leo hajawahi fungua mdomo kwa Bunge, hakuna ustawi wowote katika maendeleo yote katika eneo letu. Ikiwa 1/3 hiyo itapeleka petition, kutafanywa uchunguzi na parliament speaker ataweka kamati ya parliament kufanya uchunguzi katika huyo mbunge na ikidhibitika huyo pia anaondolewa. Sawa?

Na mwisho kabisa habari ya ID tushazungumza. ID na passport ni haki ya mwananchi, ni haki ya raia sikuwa utaenda ukaambiwa hakuna, ni haki yako na kuna njia nyingi ya kutetea haki yako, kuna Tume ambayo haki yake ni kutetea wananchi, kuna position moja inaitwa public protector au ombudsman unaweza enda kwake ukashtaki mimi mpaka leo sijapata hii na hii. Uchunguzi utafanywa na ikiwa ni haki yako kuipata wewe raia utaipata hiyo.

Mara sasa Bi. Dulu hatufikirii mambo ilivyo sasa, tunataka kubadilisha na tumeweka hapa kanuni ambayo itatuepusha na mambo kama hayo. Sawa? Campus intake pia tumesema kuwe na uwadhilifu katika kuwapa nafasi wananchi kupata elimu kwa hivyo ikiwa kuna tatizo lolote, malalamiko yeyote lazima yatachunguliwa na tume kama hicho ambazo tume … mtu anaweza kupeleka list aseme tazameni list hii. Idadi kubwa inatoka eneo hii, eneo hili hakuna wa kuenda university au idadi ya wale wamequalify ni wengi lakini waliopata nafasi sasa ni kidogo. Uchunguzi utafanywa na mambo itarekebishwa. Lakini muhimu kwa kila moja wetu ni kujua haki zake ndiyo tukasema kwamba mtu asome hii huu mswaada wa katiba aisome vizuri ajue haki zake ni ipi na ni njia gani kufuata ikiwa haki hizo zitanyimwa. Elimu ya raia, elimu katika mambo haya katiba n.k. ni kazi kubwa kwa kila mwananchi kujielemisha, kuelemisha watoto wake, jamaa zake, eneo lake n.k. Na kila kiongozi ni wajibu wake pia si kuwatumia watu katika eneo lake kujipeleka yeye mwenyewe na kutajilika na kutumikia wananchi. Na wale ambao ni watumishi wa wananchi na hawatumikii wananchi wanaweza kuondolewa wengine wakawekwa.

Mwishowe kabisa mujue kuwa raia, watu ndiyo ambao ni muhimu katika hii katiba. This was the people driven Constitution imepelekwa na wananchi na itapelekwa na wananchi na wananchi ndiyo watakao hukumu hii katiba katika conference hii yetu kubwa. Ni nyinyi kujua haki zenu na kupigania haki zenu. Nafikiri ni hayo tu, sote tumechoka kukaa, umekuwa ni muda mrefu, nimekuwa nikizungumza sana zaidi ya saa tatu, na ningependa sasa kufunga hiki kikao. Nawashukuru sana nyote mliokuja, waliosikiza, wale walioshiriki kwa kuuliza maswala pia na kama mwonavyo tumesajiri maneno yenu, na ni muhimu sasa walio wajumbe wenu ambao watakuja kwenye hii mkutano kujua kusudi ya hii katiba itakuwa ni nini ni huu mkutano ndio watakata shauri ikubaliwe. Ibadilishwe wapi, iwachwe wapi na kadhalika. Tuombe kwamba mwishowe tutapata katiba ambayo sisi twastahili kupata ambayo italinda haki zetu, itatupa demokrasia na itatupa utumishi ambao twatarajia kwa serikali yetu na viongozi wetu. Asanteni sana, Mungu awabariki natumalize sasa kwa maombi kama tulivyo fungua. Asanteni sana. (clapping)

**District Coordinator:** Mimi naona makofi hayo haikutosha kwa sababu mnaona mambo ya katiba haya ni mengi na ni marefu na yanataka muda kuelewa. Lakini nafikiri leo kama vile Bw. Idda Salim alivyofanya ameeleza kwa makini na tumeelewa kama kuna maswali zaidi tunawapatia karatasi kabla hawajaondoka tafadhali hakikisha maswali yako umeyandika na umeyachukua. Bw. Idda Salim, Commissioner ni nataka kusema hivi kwamba leo nimeona Garsen tuna bahati kwa sababu tuna mwenzetu Bwana Danson Buya Katana ambaye alichaguliwa delegate kuenda kwa National Constitutional Conference kutoka Garsen. Wako watatu, mmoja ni yeye na wawili wako katika constitutency nyingine. Kwa hivyo mimi ninasema, ninashukuru pia kwamba yeye amekuja, alikuja kuwa pamoja nasi, na bila shaka mtakuwa naye kule Nairobi. Basi kabla hatujamaliza, zile draft mlizopewa, siku ile tulikuwa na mkutano hapa, tafadhali mkiwa nazo kule mjaribu, kama hujui kusoma Kiingereza, kwa bahati baya zimeandikwa Kiingereza, zile za Kiswahili hatujazipata nadhani zitakuwako. (interjection: halafu tutawagawanyia) Kwa hivyo kama mnazo zile nilimganyia za Kiingereza kama una mtoto pale manyatta yako ambaye anajua Kiingereza, mwambie akusomee na akuelezee. Kwa sababu hii ni katiba yetu. Kwa hivyo kabla hatujamaliza ningependa tumpigie makofi tatu yenye nguvu, Commissioner wetu na wageni wake kabla hawajaondoka. Tuko tayari? Moja (clapping) Pili, (clapping) Tatu, (clapping) Asante sana na tunawatakia safari jema. Wale ambao mtaenda mjue kwamba tarehe kumi na saba pia atakuwa Hola, tarehe kumi na saba kwa hivyo muambiane wale watasafiri kuenda huko wamekosa kufika hapa wanaweza kufika pale Galole. Na tumeona msiende na njaa, tumewatengenezea kitu kidogo, nafikiri mtaonyeshwa kwa hivyo usiende na njaa, ukitoka hapa nenda ukapate kitu halafu urudi zako nyumbani. Mtaonyeshwa pale town mahali tulipowatengenezea kitu. Kwa hivyo asanteni sana. (clapping)

Meeting ended at 1.00 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&